

YESU NA SHERIA (MWALIMU)



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Nne

YESU NA SHERIA

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

(MWALIMU)

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Nne

**Africa Coordinated Curriculum for
Bible Study**

J3 - 4Ts

Used by permission of International Publications Services

**Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI**

• Copyright, 1987
Baptist Publications House
All rights reserved

YALIYOMO

SURA

UKURASA

Ujumbe Kwa Mwalimu

1. Mungu Anawaita Watu Wake	5
2. Mungu Anawaongoza Watu Wake	11
3. Mungu Anawaokoa Watu Wake	16
4. Mpende Mungu	22
5. Mungu Anataka Ibada ya Kweli	27
6. Uwe Mwaminifu Katika Ibada	31
7. Matumizi Mema ya Sabato	35
8. Waheshimu Wazazi Wako	39
9. Kuchukia ni Dhambi	44
10. Yesu Anawasamehe Wenye Dhambi	48
11. Kuiba ni Dhambi	53
12. Sema Ukweli Kila Mara	57
13. Hatupaswi Kuwa Wachoyo	60

UJUMBE KWA MWALIMU

Pengine wanafunzi wako wamejifunza Biblia tangu walipokuwa watoto. Wanaweza kuwa wanafahamu hadithi nyingi za Biblia. Lakini Je! wanaelewa hasa ukweli wa ujumbe wa Biblia?

Masomo matatu ya kwanza ya kitabu hiki ni ya kuwasaidia wanafunzi wako kuona Biblia kama kitabu kimoja. Masomo haya yanapaswa kuwasaidia waelewe vyema ukweli wa ujumbe wa Biblia.

Masomo mengine kumi yatawasaidia kuelewa maana ya Amri Kumi na jinsi Yesu alivyofafanua amri hizi.

Masomo haya yote ni ya muhimu. Utapaswa kujifunza mengi ili ujitayarishe kufundisha. Fikiria wajibu mkubwa ulionao kama mwalimu!

Unatumiwa na Mungu kuwasaidia watoto kuelewa Biblia na mpango wa Mungu kwa maisha yao.

Usiifikirie kazi yako ya ualimu kuwa si ya muhimu. Inaweza kuwa kazi muhimu sana ambayo mtu anaweza kuwa nayo. Inahitaji bidii yako. Inahitaji uwezo na nguvu ambazo Mungu tu ndiye awezaye kuzitoa kwako kupitia kwa Roho wake.

Utapaswa kukumbuka kifungu hiki cha 2 Timotheo 2:15 unapotayarisha masomo haya. "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."

SURA YA KWANZA

MUNGU ANAWAITA WATU WAKE

MASOMO YA BIBLIA: Kumbu-kumbu la Torati 6:20-25; 26:16-19

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Kusudi la masomo ya kwanza matatu katika kitabu hiki ni kuwasaidia wanafunzi wako kuelewa hasa ujumbe mkuu wa Biblia. Biblia inasimulia kuhusu upendo na jinsi Mungu alivyomshughulikia mwanadamu, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Biblia yote ina kiini kimoja -- jinsi Mungu anavyowakomboa watu wake. Ni huzuni kwamba watu wengi hawaioni Biblia kwa ujumbe mmoja. Wanakumbuka tu hadithi mbalimbali na matendo yaliyotokea. Kusudi lako si kutoa muhtasari wa hadithi na matendo yaliyofanyika unapofundisha masomo ya kwanza matatu. Bali ni lazima usisitizie ukuu wa Mungu, jinsi alivyomwumba mwanadamu na akatoa njia ya wokovu wakati mwanadamu alipofanya dhambi.

Masomo haya yanaweza kutumiwa na watoto au vijana. Panga funzo yako ili uweze kutimiza mahitaji na uelewaji wa kundi unalofundisha.

Ushirika wa Mungu na mwanadamu una msingi wake katika maagano waliyofanya pamoja. Majina ya sehemu mbili za Biblia, Agano la Kale na Agano Jipya, yanaonyesha ukweli huu. Twasoma kuhusu agano la Mungu na watu wake katika Biblia yote.

Agano ni mapatano. Kulingana na jamii, agano huwa ni mapatano kati

ya watu wawili. Kulingana na Maandiko, neno "Agano" linaeleza ushirika wa mwanadamu na Mungu. Biblia ni hadithi ihusuyo agano la Mungu na watu wake.

Biblia inaeleza Agano ambalo Mungu alifanya na watu wake, Israeli. Aliwaambia wamtii na wamfuata naye angewakomboa. Angewarudisha katika ushirika mwema naye. Angetumia Israeli kuleta ukombozi kwa watu wote wa ulimwengu.

Watu wa Mungu walishindwa kutekeleza wajibu wao wa kutimiza agano. Lakini Mungu hakuacha kushirikiana nao. Alifanya "agano jipya" nao. Alikuwa ulimwenguni kupitia kwa Yesu Kristo ili atuokoe sote, watu wake.

Soma Maandiko yote ya Biblia uliyopewa unapojiandaa kufundisha somo hili. Unapofundisha utapaswa kueleza historia ya Waisraeli hadi walipokuwa jangwani. Usieleze kwa moja moja lakini ujaribu kueleza mambo yaliyomuhimu.

Andika kwenye karatasi au ubaoni mambo yafuatayo:

1. Mungu aliuumba ulimwengu na vyote vilivyomo.
2. Mwanadamu aliamua kutomtii Mungu na akajitenga na Mungu.
3. Mungu alimwita Ibrahimu na akaanza mpango wake wa kumrudisha mwanadamu kwake.

4. Mungu aliwakomboa Waisraeli kutoka utumwani kule Misri.
5. Mungu aliwapa Waisraeli Amri Kumi ambazo zinaeleza wajibu wa Israeli kwa Mungu na kwa mwanadamu.

Zungumzia kila mojawapo ya mambo haya ili wanafunzi waweze kuona picha kamili ya wakati huo ya maisha ya watu wa Mungu. Usiitupe karatasi hiyo ambayo umeandika madokezo haya. Iweke ili kwamba uweze kuongezea mambo mengine wiki ijayo.

Tumia Maandiko uliyoweka kueleza juu ya kutolewa kwa Amri Kumi hizi. Waisraeli walikuwa wametolewa utumwani. Mungu alikuwa akiwafanya wawe taifa. Upendo wa Mungu ulitarajia kwamba watu hawa waitikie kwa kutimiza kusudi lake kwao. Mungu aliwapa amri hizi ili kuwaonyesha kile walichopaswa kufanya. Amri hizi zilidhihirisha wazi wajibu wao kwa Mungu na wajibu wao kwa mwanadamu. Mungu alikuwa ameagana na watu wake.

Kumbukumbu la Torati 6:20-25 inasema jinsi watu hawa wawezavyo kuwaeleza watoto wao kitendo hiki cha agano.

Soma kwa makini vifungu hivi vyote unapoandaa somo. Utapaswa kuwaeleza wanafunzi kwa lugha rahisi unapowafundisha.

Hakikisha kwamba umetilia mkazo mambo yafuatayo unapofundisha:

1. Mungu aliuumba ulimwengu na mwanadamu. Muumbo wa

Mungu ulikuwa mzuri, lakini mwanadamu aliamua kutomtii Mungu. Kutotii huku kunaitwa dhambi na dhambi ilimtenganisha mwanadamu na Mungu.

2. Mungu ana mpango wa kumrudisha mwanadamu kwake. Mpango huu unajulikana kama "ukombozi".
3. Mungu alianza mpango huu kwa kushirikiana na kundi la watu waitwao Waisraeli. Aliwaokoa kutoka utumwani kule Misri na akaagana nao. Walipaswa kumtii na pia kutii amri zake. Angewatumia kwa kuukomboa ulimwengu wote.

KUSUDI LA SOMO HILI:
Kuwawezesha wanafunzi kuelewa Biblia kama rekodi ya tukio la Mungu la kuwakomboa wanadamu.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! kuna milima mahali unapoishi? Ikiwa ipo, Je! umewahi kupanda juu ya mojawapo ya milima hii? Je! huweza kuona nini ufikapo juu ya milima hii? Ndiyo, unaweza kuona vitu vilivyoko chini yake: misitu, mito na kila kitu! Kila kitu huonekana kuwa kidogo sana. Navyo vyote huwa kama picha moja.

Kila kitu huonekana tofauti kwa sababu u juu ya mlima huo. Hukiangalii kitu kimoja bali sehemu kubwa ya nchi.

Sema: Je! Biblia ni nini? (Wanyeshe Biblia yako unapowauliza swali hili. Ngojwa wajibu kabla ya kuwajibu.)

Sema: Biblia ni hadithi ihusuyo jinsi Mungu alivyoshirikiana na mwanadamu ili kumrudisha katika ushirika mwema naye.

Tumia orodha uliyoandika yenye mambo matano yanayoonyesha jinsi Mungu alivyofanya kazi ulimwenguni. Au yaandike ubaoni unapoeleza kila moja.

Wasomee wanafunzi hao sentensi ya kwanza:

1. Mungu aliuumba ulimwengu na vyote vilivyomo.

Waambie wanafunzi hao watafute Mwanzo 1:31. Mchague mmoja wao asome kifungu hiki. Sema: Mwandishi wa kitabu cha Mwanzo anatwambia kwamba Mungu aliuumba ulimwengu wote na anatawala kila sehemu yake. Alimwumba pia mwanadamu. Alimpa mwanadamu uhuru wa kumtii au kutomtii.

Uliza: Je! mwanadamu alichagua nini? (Kutomtii.)

Waonyeshe sentensi ya pili (au iandike ubaoni):

2. Mwanadamu aliamua kutomtii Mungu na akatengana na Mungu.

Sema: Kutotii kwa mwanadamu kunaitwa dhambi. Dhambi iliharibu ushirika mwema uliokuwepo baina ya Mungu na mwanadamu. Hata hivyo, Mungu yungali anapambana kushinda maovu. Yungali anafanya kazi ya kuwarudisha wanadamu na ulimwengu kwake.

Weka mkono wako wa kushoto katika Biblia mwanzoni mwa kitabu

cha Mwanzo na mkono wako wa kulia katika mwisho wa kitabu cha Ufunuo. Sema: Je! mnaona kurasa hizi zote za Biblia? Zote zinazungumzia jinsi Mungu anavyojishughulisha kumrudisha mwanadamu katika ushirika mwema naye.

Waambie wanafunzi hao wafungue katika Ufunuo 21:6-8 na 22:3-4 na uwachague wanafunzi wawili wa kusoma vifungu hivi. Sema: Vifungu hivi vinatwambia kwamba Mungu atapata ushindi hata ingawa kuna uovu ulimwenguni.

Sema: Agano Jipya inatwambia jinsi Mungu alivyomtuma Yesu Kristo kuzichukua dhambi zetu. Kitabu hiki cha Ufunuo kinatwambia maovu yatashindwa wakati wa mwisho na kusudi nzuri la Mungu litatimizwa.

Sasa ishike Biblia yote mikononi mwako. Sema: Biblia ni rekodi jinsi Mungu alivyojishughulisha ulimwenguni ili kumkomboa mwanadamu.

Uliza: Je! Mungu anafanyaje kazi yake? Je! huifanya kupitia kwa watu?

Sema: Ndiyo, Mungu amekuwa akifanya kazi kupitia kwa watu. Aliwachagua Waebrania miaka mingi iliyopita. Aliwaita ili wamtii. Alijidhihirisha kwao kwa njia maalum. Aliwaita pia kushiriki ufahamu wao wa Mungu na watu wengine wa ulimwengu.

Uliza: Je! mnafikiri kwamba Mungu anawataka watu wote wa ulimwengu kujua upendo wake na mpango wake wa ukombozi? (Ndiyo)

Sema: Sasa, hebu tujaribu kuelewa jinsi Mungu alivyofanya kazi kupitia kwa Waebrania.

Waonyeshe sentensi ya tatu:

3. Mungu alimwita Ibrahimu na akaanza mpango wake wa kumrudisha mwanadamu kwake.

Sema: Mungu alimwita kwanza mtu mmoja ili kufanya kazi katika Waebrania. Jina la mtu huyu ni Ibrahimu. Mungu alifanya agano na Ibrahimu.

Uliza: Je! agano ni nini? (Tazama elezo lililoko katika sehemu ya "kujiandaa kufundisha" na uzungumzie elezo hilo.)

Eleza kwamba Mungu alipatana na Ibrahimu kwamba angemtumia kuubariki ulimwengu wote. Mungu angambariki Ibrahimu naye angekuwa baraka kwa wengine. Kitabu cha Mwanzo kinazungumzia habari za Ibrahimu.

Waonyeshe sasa sentensi ya nne:

4. Mungu aliwaokoa Waisraeli kutoka utumwani kule Misri.

Sema: Uzao wa Ibrahimu walifanywa watumwa kule Misri baada ya miaka mingi kupita. Mungu alikuwa akifanya kazi ulimwenguni alipowakomboa Waisraeli kutoka utumwani. Kiongozi wao alikuwa mtu aitwaye Musa. Mungu alimwambia Musa na watu hao kwamba angewaongoza hadi kwa nchi nzuri ambako wangukuwa taifa kuu.

Mungu alikuwa mwaminifu kwa kutimiza agano lake na watu wake.

Hata ingawa walifanya dhambi na kumwasi hakuacha kuwapenda na kuwaonyesha njia ya haki ya kufuata.

Waonyeshe sentensi ya tano:

5. Mungu aliwapa Waisraeli Amri Kumi ambazo zinaeleza wajibu wa Israeli kwa Mungu na mwanadamu.

Sema: Sehemu ya ajabu ya mpango wa Mungu kwa watu aliowapenda ulikuwa kuwapa Amri Kumi. Alijua kwamba walihitaji sheria fulani za kuwaongoza. Sheria hizi au amri zilikuwa za kuwaongoza na kuwaonyesha wajibu kwa Mungu. Walikuwa pia na wajibu kwa watu wanaoishi nao. Amri Kumi zilidhihirisha wazi wajibu wao kwa Mungu na kwa mwanadamu.

Sema: Baadhi ya vifungu katika Kumbukumbu la Torati 6 vina-twambia yale ambayo Mungu alikuwa akifanya wakati alipowatoa watu wake kutoka Misri.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Kumbukumbu la Torati 26:16-19. **Sema:** Mungu alikuwa akiwafanya Waebrania kuwa taifa. Alitaka kulitumia taifa la Israeli kwa kuubariki ulimwengu wote.

Uliza: Je! mnafikiri ni kwa nini Mungu aliwapa watu hawa amri hizi? (Ngoja majibu.)

Sema: Mungu aliwapa amri hizi ili kuwaonyesha yale waliyopaswa kufanya. Amri hizi ziliwaambia jinsi walivyopaswa kushiriki na Mungu pamoja na wanadamu wengine.

Sema: Hebu tusome Kumbukumbu la Torati 6:20-25. Vifungu hivi vinatwambia jinsi watu hao wangewaelezea watoto wao amri hizi. (Mchague mwanafunzi mmoja asome vifungu hivi au waweza kuvisoma wewe mwenyewe.)

Sema: Wiki ijayo tutajifunza mengi kuhusu jinsi Mungu alivyofanya kazi kupitia kwa Waebrania. Lakini tuisahau kwamba ujumbe muhimu wa Biblia inahusu jinsi Mungu alivyofanya kazi ulimwenguni ili kuwarudisha watu katika ushirika mwema naye mwenyewe.

Wasaidie wanafunzi wajibu maswali yaliyo katika sehemu ya "Kazi ya Kufanya". Pengine watataka msaada wa kuandika tafsiri ya Biblia. Tafsiri ambayo wanafunzi watatoa haipaswi kuwa kama ile iliyotolewa. Lakini inapaswa kulingana.

KAZI YA KUFANYA

Kuna usemi hapa chini uhusio Biblia. Andika herufi ya S kando ya sentensi zilizo za kweli na herufi K kando ya sentensi zisizo za kweli.

S Biblia ina sehemu mbili, nazo ni Agano la Kale na Agano Jipya.

K Ujumbe wa Agano la Kale na Agano Jipya hauhusiani hata kidogo.

S Biblia ni rekodi jinsi Mungu alivyofanya kazi ya kuukomboa ulimwengu.

S Amri kumi ni mwongozo wa kutuonyesha jinsi ya kuishi.

Kwa kuyatumia maneno yako tu andika katika nafasi ifuatayo maana ya Biblia: Biblia ni rekodi inayohusu jinsi Mungu anavyofanya kazi ulimwenguni ili kumrudisha mwana-damu katika ushirika mwema naye mwenyewe.

Andika maana ya neno "agano."

Agano ni mapatano kati ya sehemu mbili. Kulingana na Biblia, agano ni mapatano ambayo Mungu anafanya na mwanadamu.

Kunayo maneno magumu katika somo hili. Jifunze maana ya maneno yafuatayo:

Waebrania...Hili ni jina lingine la Wayahudi, jina la lugha ya Kiyahudi.

Israeli...Taifa la Wayahudi, jina lingine la Yakobo.

Agano...Agano ni mapatano. Kulingana na jamii agano hufanywa baina ya watu wawili. Kulingana na Maandiko neno "agano" linaelezea ushirika wa mwanadamu na Mungu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Naye Bwana amekuungama hivi leo kuwa taifa iliyotengwa iwe yake yeye, kama alivyokuahidi, na kuwa yakupasa kushika maagizo yake yote" (Kumbukumbu la Torati 26:18).

Mungu alipofanya agano na Israeli aliahidi kuwabariki na kuwatumia kuubariki ulimwengu wote. Aliwapa

amri ili wawe na mwongozo jinsi ya kuishi. Mara kwa mara Israeli ilikosa kutii na kuvunja amri hizi, lakini Mungu hakuwaacha. Agano lake lilikuwa agano la neema. Mungu alimtuma Yesu, walipotumia vibaya sheria na kuifanya kuwa ya maana sana kuliko watu. Yesu hakuja kuipinga sheria bali kuitimiza. Alikuwa kuwakomboa watu kutoka dhambini.

WAKATI WA MWISHO

Tumia mtindo wo wote utakao kufundisha kifungu cha kukumbuka. Pengine unaweka rekodi ya wale ambao wanaweza kusema vyema kifungu hicho kila Jumapili.

Soma tena kusudi la somo hili. Kusudi hili ndilo litakalotumiwa katika masomo haya yote matatu. Utakuwa umetimiza sehemu moja ya kusudi hili iwapo wanafunzi wanaelewa kwamba kitabu cha Mwanzo na Kutoka vinaeleza jinsi Mungu alivyoanza kushirikiana na Mwanadamu. Alikuwa akishirikiana naye ili amkomboe kutoka dhambini (amrudishe mwanadamu katika ushirika mwema naye mwenyewe).

Endelea kueleza wakati wa mwisho jinsi Mungu yungali anafanya kazi ulimwenguni siku hizi. Ana kazi ambayo anamtaka kila mmoja wetu afanye jinsi alivyowapatia Ibrahimu na Musa. Eleza kwamba Mungu anataka kutumia kila Mkristo kwa kuwaambia wengine ujumbe wa ukombozi. Anatutaka tueneze ujumbe huu katika kila sehemu ya ulimwengu. Waambie wanafunzi wafikirie kile ambacho Mungu anawataka wafanye wiki ijayo.

SURA YA PILI

MUNGU ANAWAONGOZA WATU WAKE

MASOMO YA BIBLIA: Yeremia 31:31-34

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! wanafunzi wako waliitikiaje somo la wiki iliyopita? Je! lilikuwa ngumu kwao kuelewa? Je! ulipata ugumu kulifundisha? Ikiwa lilikuwa ngumu, basi unahitaji kufanya bidii wakati huu ili liwe rahisi. Mwombe Mungu akuongoze unapojiandaa.

Liangalie tena kusudi la somo hili. Ni sawa na lile la wiki iliyopita: kuwawezesha wanafunzi kuelewa Biblia kama rekodi ya tukio la Mungu la kuwakomboa wanadamu. Hauwezi kutimiza kusudi hili katika somo moja tu, kwa hivyo limetolewa katika masomo matatu.

Somo hili la pili litawasaidia wanafunzi kujifunza kwamba Biblia inasimulia jinsi Mungu alivyo-waongoza watu wake. Aliwaongoza Waebrania kutoka utumwani kule Misri na kuwa huru katika Nchi ya Ahadi. Alifanya hivi kwa sababu alitaka awatumie kwa kuubariki ulimwengu. Mungu alitaka atumie taifa la Israeli katika mpango wake wa kuukomboa ulimwengu.

Wanafunzi hawatafurahia somo hili iwapo hautalinganisha mafunzo hayo na maisha yao. Wanapaswa kutambua kwamba tutakuwa na shida wakati Mungu anapotuelezea wazi njia ya kufuata, lakini sisi tunakataa kufuata njia hiyo. Israeli ilitaka kuwa taifa kubwa badala ya kutumiwa na Mungu

ili kuleta wokovu ulimwenguni. Waebrania walijiletea wenyewe hukumu ya Mungu kwa kutokutii kwao.

Ongezea wiki hii juu ya mambo muhimu ya historia ya Israeli. Wiki iliyopita uliorodhesha mambo matano. Wiki hii utaongezea mambo haya yafuatayo:

6. Mungu aliwaongoza Waisraeli hadi Kanaani, Nchi ya Ahadi.
7. Israeli haikufuata mpango wa Mungu aliowapa na baada ya miaka mingi kupita walishikwa mateka na nchi zingine na kwenda kuishi uhamishoni.
8. Mungu aliendelea kuwapenda watu wake hata ingawa walikosa kumtii. Alisema kwamba angefanya jambo jipya na kuwarudisha tena Yerusalemu.

Utapaswa kusoma sura zifuatazo katika Biblia yako iwapo hufahamu vizuri historia ya Waisraeli hadi wakati huu. Soma Yoshua 1, Waamuzi 2, 1 Samweli 8, 2 Wafalme 17:1-18, 25:1-12. Maandiko haya yatakusaidia uelewe kile kilichofanyika baada ya Israeli kupelekwa Kaanani.

Maandiko ya somo la leo yanapatikana katika Yeremia 31:31-34. Yaliandikwa na mmojawapo wa manabii wa Mungu ambaye alimwita ili awaonye watu wake juu ya kutotii kwao. Kuna ujumbe wa

matumaini katika vifungu hivi. Taifa la Israeli halikuwa limetii agano la Mungu, na, kwa hivyo taifa lenyewe lilikuwa limeangamizwa. Watu walikuwa wameshikwa mateka na kupelekwa Babeli. Yeremia alisema kwamba Mungu alikuwa yungali na watu wake hata ingawa walikataa kumtii. Angeendelea kuwaongoza, na angeagana upya nao.

Je! ni nini kipya kuhusu agano hili? Halingekuwa agano la sheria ya kwanza, bali lingekuwa ahadi. Roho wa Mungu angeishi miyoni mwa watu wake. Angewasamehe na kusahau dhambi zao. Fungu hili linaelekeza kwa Agano Jipya na kuja kwa Kristo.

Hakikisha kwamba unalitia mkazo ukweli ufuatao unapofundisha:

1. Mungu alikuwa mwaminifu kutimiza agano lake na watu nao hata ingawa walishindwa na kufanya dhambi.
2. Watu wa Mungu walijiletea hukumu wao wenyewe walipokataa kufuata uongozi wake.
3. Mungu hatawaacha watu wake bila tumaini. Atawasamehe dhambi zao na aishi ndani yao kupitia kwa Roho wake.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwawezesha wanafunzi kuielewa Biblia kama rekodi ya tukio la Mungu la kuwakomboa wanadamu.

KULIFUNDISHA SOMO

Inua juu Biblia yako. Sema: Wiki iliyopita mliandika fafanuzi la kitabu

hiki. Je! mnakumbuka jinsi mlivyoieleza Biblia? (Ngojia majibu na urudie yale uliyofundisha wiki iliyopita yahusu Biblia: Ni rekodi inayohusu jinsi Mungu anavyofanya kazi ulimwenguni ili kumrudisha mwanadamu katika ushirika mwema naye mwenyewe.)

Weka mkono wako wa kushoto katika mwanzo wa kitabu cha Mwanzo na mkono wako wa kulia katikati ya kitabu cha Kutoka. Sema: Wiki iliyopita tulizungumzia kuhusu kile kilichofanyika katika sehemu hii ya Biblia. Sasa weka mkono wako wa kushoto katikati ya kitabu cha Kutoka na mkono wa kulia katika mwisho wa Agano la Kale. Sema: Leo tutazungumzia mengi yaliyofanyika katika sehemu hii ya Biblia. Kumbuka kwamba, itakuwa jinsi uonavyo bonde ukiwa juu ya mlima. Utaona sehemu yote badala ya mahali pamoja tu.

Bandika orodha yako ukutani na uwaonyeshe sentensi ya 6: Mungu aliwaongoza Waisraeli hadi Kanaani, Nchi ya Ahadi.

Uliza: Je! nani awezaye kutwambia yule mtu aliyewaongoza Waisraeli kutoka utumwani kule Misri? (Musa)

Tumia habari ifuatayo kusimulia hadithi hii jinsi Mungu alivyo- waongoza watu kutoka jangwani. Usisome hadithi hii, bali isimulie.

Miaka waliyokuwa jangwani ilikuwa ya shida nyingi. Ilikuwa ya shida hasa kwa Waisraeli. Ilikuwa ya shida pia kwa Musa. Musa alikuwa mvumilivu sana na watu hawa. Walikuwa wakiasi kila mara na kutoshukuru. Wao walimlaumu Musa mara kwa mara.

Watu hawa walihitaji sana maji. Siku moja walianza kulalamika walipokosa maji. Walimlaumu Musa kwa kuwatoa Misri. Mungu alimwambia Musa anene na jabali (mwamba) nayo maji yangeweza kupatikana. Lakini Musa alikuwa amekasirishwa sana na watu hao. Badala ya kusema na jabali (mwamba) hilo, alilipiga mara mbili kwa fimbo yake. Mungu naye hakumruhusu kuiingia Nchi ya Ahadi kwa sababu alikosa kumtii.

Kizazi chote cha Waisraeli walifia jangwani. Mwishowe Musa na wale vijana vijana waliobakia walifika katika eneo la Moabu. Musa alipanda juu ya mlima Nebo na akaiangalia Nchi ya Ahadi. Alijua kwamba hangeruhusiwa kwenda na kuimiliki nchi hiyo pamoja na wengine. Hata hivyo, AGANO hili lingetimizwa hata ingawa kizazi chote kilifia jangwani. Mungu aliikumbuka ahadi yake hata ingawa alipaswa kuwachagua viongozi waya.

Sasa waonyeshe sentensi ya saba:

7. Israeli haikufuata mpango wa Mungu aliowapa na baada ya miaka kupita walishikwa mateka na nchi zingine na kwenda kuishi uhamishoni.

Endelea kusimulia hadithi hii:

Mtu aitwaye Yohana aliwaongoza Waisraeli hadi kwa Nchi ya Ahadi. Nchi ya Kanaani ilishindwa na kugawanywa kati ya makabila ya Israeli. Mungu aliwaongoza watu hawa akitumia watu waitwao Waamuzi. Mungu ndiye aliyewateua watu hawa. Hawakuchaguliwa na Waisraeli wengine. Hawakutoka kwa jamaa za kifalme. Ila, uwezo mkuu wa Mungu ulionekana maishani mwao. Watu waliwafuata walipotambua kwamba wao walikuwa wakiongozwa na mkono wa Mungu.

Watu waliweza kutambua wakati huu kwamba waliweza kubarikiwa walipokumbuka AGANO la Mungu kwao na waliposhirikiana pamoja kumtumikia Mungu na kufanya mapenzi yake. Nao waliteseka walipomwasi Mungu na kuvunja AGANO lake.

Samweli alikuwa mwamuzi wa mwisho. Alikuwa mtu mkuu sana. Watu walimwambia Samweli kwamba wanataka mfalme. Samweli aliwaonya juu ya hatari ya kuwa na mfalme. Hata hivyo, watu hawa walitaka kuwa taifa lenye nguvu na walitaka mfalme ambaye angewaongoza wakati wa vita.

Mungu alitaka kuwaondolea watoto wake mateso ambayo wangepata iwapo wangepata njia hii. Hali ukweli mkuu wa maisha hujulikana kupitia kwa mateso. Ingekuwa tu kupitia kwa mateso ambayo yalikuwa mbele yao ndipo Waisraeli wangepajifunza kuhusu neema na hukumu ya Mungu.

Jamii ya Israeli, ilikuwa taifa. Iliweza kujulikana sana na kuwa tajiri chini ya uongozi wa Mfalme Daudi. Taifa hili lilikuwa tajiri sana wakati Sulemani, mwanawe Daudi, alipotawala. Lakini kulikuwepo na kutotosheka kwingi na mwishowe ufalme huu uligawanyika na kuanzisha ufalme wa Kaskazini na Kusini.

Ufalme wa Kaskazini uliangamizwa na Waashuru mnamo mwaka wa 722 B.C. Nao ufalme wa kusini uliangamizwa na Wababeli mnamo mwaka wa 587 B.C. Watu hawa walishikwa kama mateka.

Mungu aliwaita watu wa kunena na Waisraeli katika wakati huu wa shida. Watu hawa waliitwa manabii. Walijaribu kuwaonyesha watu sababu ya shida walizokuwa wakipata. Waliwaonya watu juu ya matokeo ya matendo yao maovu. Manabii hawa walitabiri juu ya kuharibiwa kwa Yerusalemu na Hekalu.

Waonyeshe sasa sentensi ya 8 katika orodha yako: Mungu aliendelea kuwapenda watu wake hata ingawa walikosa kumtii. Alisema kwamba angefanya jambo jipya na kuwarudisha tena Yerusalemu.

Mchague mwanafunzi mmoja asome Yeremia 31:31-34 wakati wengine wanapofuata habari hii katika Biblia zao.

Uliza: Je! ni nani aliyeandika maneno haya? (Yeremia) Je! Yeremia alikuwa nani? (Nabii)

Sema: Israeli ilikuwa imekosa kumtii Mungu. Nao hawangeepuka matokeo ya yale waliyokuwa wamefanya. Mungu alikuwa amewaonya watu wake kupitia kwa manabii, lakini watu hao hawakumsikiliza kamwe. Taifa hili liliangamizwa. Watu hawa walishindwa na mataifa mengine.

Uliza: Je! mnafikiri kwamba Mungu aliwasahau watu wake na akawaacha? (La, aliendelea tu kuwapenda na kuwa pamoja nao.)

Sema: Hata ingawa watu hawa walikuwa wamevunja agano ambalo Mungu alikuwa amefanya nao, Yeremia aliwaambia kwamba Mungu angefanya *agano jipya* nao. Angewasamehe dhambi zao na angekuja kuishi mioyoni mwao kupitia kwa roho wake. Yeremia hakuamini kwamba Mungu angepaacha watu wake. Ujumbe wake ulikuwa kwamba Mungu angeendelea kufanya kazi kupitia kwa Israeli. Tutaona jinsi Mungu alivyofanya jambo hili wiki ijayo.

Wasaidie wanafunzi na kazi ya kufanya iliyoko katika vitabu vyao. Sahihisha majibu yao.

KAZI YA KUFANYA

Hapo chini kuna picha za watu ambao wametajwa katika somo hili la leo. Chini ya picha hizo kuna usemi uhusuo watu hao. Andika jina la mtu yule kando ya sentensi inayoeleza habari zake.

MUSA Aliwaongoza Waisraeli kutoka Misri hadi Nchi ya Ahadi.

YOSHUA Aliwaongoza Waisraeli kuingia katika Nchi ya Ahadi.

SAMWELI Alikuwa mwamuzi wa mwisho wa Israeli.

DAUDI Alikuwa mmoja wapo wa Wafalme wakuu wa Israeli.

YEREMIA Alikuwa nabii ambaye aliandika Maandiko ya Biblia ya somo letu la leo.

Jifunze maana ya maneno haya:

Waamuzi...Hawa walikuwa wazee waliochukua uongozi wakati Waisraeli walipovamiwa au kutishwa na majeshi ya nchi zingine walipoishi Palestina.

Mateka ... Huu ulikuwa wakati wa kuishi utumwani, wakati Wayahudi walioshindwa (wapatao elfu hamsini)

walishikwa na kuishi Ashuru na Babeli. Kipindi hiki kilichukua muda wa miaka hamsini, lakini Waebrania wengi hawakurudi kwao.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana: Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitalandika, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu" (Kumbukumbu la Torati 31:33).

Manabii wa Agano la Kale walizungumzia mara kwa mara kuhusu maagano ambayo Mungu alikuwa amefanya na watu wake. Yeremia katika kifungu cha 31 amesema kwamba Mungu ataagana upya na watu wake. Agano hili lingemandikwa katika mioyo yao. Nalo lingeanzia kwa msamaha na ushirika wa mtu na Mungu. Lingekuwa agano la neema. Baada ya miaka mia sita kupita tangu Yeremia aliposema maneno hayo, Yesu naye aliwaambia wanafunzi wake kwamba, "Hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi" (Marko 14:24). Alikuwa akiwaambia kwamba alikuwa anatimiza ahadi ya kale iliyotolewa kwa Yeremia - sasa kulikuwepo na Agano Jipya.

WAKATI WA MWISHO

Linganisha yale yaliyofanyika kwa Israeli na yale yanayofanyika kwetu siku hizi tunapokosa kutii.

Sema: Sisi tulio Wàkristo tumefanya agano na Mungu. Alimtuma Yesu kufa kwa ajili yetu. Yesu alifufuliwa kutoka kwa wafu. Ametupa maisha mapya. Roho wa Mungu yuaishi ndani yetu. Mungu alifanya kuwepo kwa agano hili. Schemu yetu ya mapatano haya ni kuishi kwa ajili yake kwa kumruhusu aishi ndani yetu.

Sema: Wiki ijayo tutaona jinsi Biblia inamalizia schemu iliyobakia ya hadithi jinsi Mungu anavyofanya kazi na watu wake.

Funga kwa maombi.

SURA YA TATU

MUNGU ANAWAOKOA WATU WAKE

MASOMO YA BIBLIA: Isaya 53:3-6; Mathayo 28:16-20

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! wanafunzi wako wanapenda mtindo huu mpya wa kuifahamu Biblia? Pengine wataona ugumu kuifikiria Biblia kama ujumbe mmoja, lakini ni muhimu kwao kujifunza kufikiria hivyo. Wanapaswa kuona hasa kiini cha Biblia kama kazi ya Mungu na mwanadamu ya kumrudisha katika ushirika mwema naye mwenyewe. Nazo walizosikia zitaweza kuwa kitu kimoja.

Fundisha kwa njia ya kuvutia jinsi uwezavyo. Wahimiza wanafunzi waulize maswali na kutoa maoni yao.

Somo la leo ni la mwisho katika mfululizo wa masomo matatu ambapo tunajaribu kuona ujumbe muhimu wa Biblia nzima. Kichwa chake ni "Mungu Anawaokoa Watu Wake." Yote ambayo Mungu alifanya tangu hapo mwanzo alifanya akiwa na nia ya kuwaokoa watu wake. Mwanadamu alifanya dhambi. Dhambi hii iliondoa ushirika mwema uliokuwepo kati ya Mungu na Mwanadamu. Mungu alianza mara moja mpango wake wa kuangamiza dhambi, ukuta ulimtenganisha mwanadamu na Mungu..

Mwanzoni kabisa Mungu aliwaita kundi la watu, yaani Israeli, na akafanya kazi kupitia kwao. Alifanya agano nao. Angewaongoza na walipaswa kumtii. Lakini Israeli

walishindwa kutii mara kwa mara. Wala watu hawa hawakuelewa wajibu wao wa kushiriki upendo wa Mungu na mataifa mengine.

Hata hivyo, Mungu aliendelea kuwatumia Waisraeli kwa sababu Yesu angezaliwa katika taifa hili. Mungu alionyesha upendo uliomkuu sana. Alikuwa ulimwenguni kama Yesu Kristo. Yesu alikuwa mtumishi na akajitwika dhambi za ulimwengu. Alikufa ili tuweze kupatanishwa na Mungu. Alikufa ili abomoe ukuta wa dhambi ambalo ulitutenganisha na Mungu.

Wote wanaoitikia upendo wa Mungu na kuwa wafuasi wake huwa ndio Israeli mpya. Israeli mpya hii ni Kanisa. Tumeamriwa kushiriki upendo wa Mungu na ulimwengu wote.

Utapaswa kudhihirisha wazi ukweli huu kwa wanafunzi unapofundisha.

Kuna sehemu mbili za Maandiko katika somo la leo. Moja inatoka katika Agano la Kale na nyingine katika Agano Jipya. Unaweza kuyafikiri kuwa ni daraja iunganishayo sehemu mbili za Biblia.

Soma Isaya 53:3-6. Isaya aliandika mashairi fulani yahasuyo "mtumishi anayeteswa." Mungu naye aliita Israeli kuwa mtumishi huyo. Lakini Israeli haikutimiza kazi ya mtumishi. Vifungu hivi pia vinaelezea aina nyingine ya mtumishi. Mungu alifanya agano lingine jipya la ahadi kwa

sababu Israeli haikutii sheria. Aliahidi kumtuma mwokozi. Mwokozi huyu angeteseka kwa ajili ya dhambi za mwanadamu.

Soma Mathayo 28:16-20. Yesu alirudi kwa Baba baada ya kutimiza kazi ambayo Mungu alimtuma afanye. Naye aliwaambia wanafunzi wake maneno haya kabla ya kwenda mbinguni. Maneno haya huwa yanajulikana kama Agizo Kuu. Yanaeleza yale ambayo watu wa Mungu, yaani kanisa, wanapaswa kufanya ulimwenguni.

Ongezea kwenye orodha yako mambo yafuatayo:

9. Mungu aliwatoa Waisraeli utumwani na kuwarudisha Yerusalemu. Waliahidi kuonyesha imani na shukrani zao kwa kutii sheria.
10. Watu hawa waliifanya sheria kuwa jambo la muhimu na la kwanza maishani mwao. Walipoteza ufahamu wa kazi ambayo Mungu aliwaitia.
11. Mungu alimtuma Yesu kufanya kile ambacho hapangekuwa na ye yote wa kukifanya. Alilipa deni la dhambi zetu.
12. Wote ambao wanamwamini Yesu kama mwokozi wao na kuwa wafuasi wake ndio Israeli mpya - kabisa. Kazi yetu ni kushiriki upendo wa Mungu na ulimwengu wote.

Pengine utataka kurudia orodha ya mambo yote ulioandika kuanzia somo la kwanza.

Utapaswa kutilia mkazo ukweli ufuatao unapofundisha.

1. Historia ndefu ya mpango wa Mungu wa ukombozi ilitimizwa katika Yesu Kristo.
2. Yesu alianzisha kanisa na wote wajao kanisani huja kwa imani katika Yesu.

KUSUDI LA SOMO HILI:
Kuwawezesha wanafunzi kuielewa Biblia kama rekodi ya tukio la Mungu la kuwakomboa wanadamu.

KULIFUNDISHA SOMO

Wachague wanafunzi wawili na uwaambie wasimame 50 centimita kutoka kwa mwenzake na wagusane mikono yao.

Sema: Hebu tuite mmoja wenu Agano la Kale, na mwingine Agano Jipya. Mnapounganisha mikono yenu pamoja, mnatengeneza "daraja" ya kutoka upande mmoja hadi mwingine. Tunataka tugundue leo daraja ambayo inaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya.

Tumia mtindo ule ule wa kusimulia hadithi ambao ulitumia wiki iliyopita. Hata hivyo, usisome yote maelezo yote yaliyotolewa. Wanafunzi wanaweza kutofurahia ukifanya hivyo. Jifunze kusimulia kwa maneno yako mwenyewe na uonyeshe vitendo katika hadithi yako.

Sema: Hebu na tuendeleo na hadithi yetu ihusuyo jinsi Mungu alivyoshiriki kikazi watu wake ili kutimiza kusudi lake.

Israeli ilivamia na kushindwa na Babeli. Watu wengi walishikwa mateka na kupelekwa Babeli. Hata hivyo, Mungu aliyetoa watu wake kutoka Misri alikuwa tayari kufanya "jambo lingine kuu". Alinena kupitia kwa nabii wake aliwaye Isaya kwa watu waliokuwa uhamishoni.

Isaya alitangaza "Habari Njema" za kuja kwa ukombozi wa Mungu. Alisema kwamba Mungu angewawezesha Waisraeli kurudi nyumbani kwao. Mungu wao angewatumia kutimiza mpango wake kwa ulimwengu.

Nebukadneza, mfalme wa Babeli alikufa. Baadaye mtu, aliwaye Koreshi alishinda Babeli. Koreshi aliwaruhusu baadhi ya watu wa Israeli kurudi Yerusalemu. Watu hawa walijenga tena kuta za Yerusalemu chini ya uongozi wa Nehemia na Ezra. Walijenga pia Hekalu. Ezra alifika akiwa na sehemu ya kitabu cha sheria na akakisoma mbele ya watu hao. Watu hao walisikitikia sana matendo yao. Walielewa kwamba kushikwa kwao kulikuwa kama hukumu ya Mungu kwao kwa ajili ya kutokuwa waaminifu. Hawakuwa wametii sehemu yao ya agano. Waliahidi kuonyesha imani na shukrani zao kwa kutii sheria.

Ni huzuni kubwa kwamba baada tu ya miaka michache kupita watu hao walifanya "kutii sheria" kuwa muhimu zaidi kuliko ushirika wao na Mungu. Walianza kufikiri kwamba wao ni bora zaidi kuliko watu wengine. Walisahau kwamba Mungu alikuwa amewaita ili washiriki imani yao na wengine.

Isaya alinena na watu. Alieleza Israeli kuwa ni "mtumishi" aliyetwa kutimiza mpango wa Mungu. Lakini Israeli ilishindwa na wakapelekwa uhamishoni. Nabii huyu anaendelea kusema kwamba Mungu atawatumia watu wachache watakaobakia ili kutimiza kazi yake. Hawa wachache ni wale waliorudi kutoka

uhamishoni. Lakini hata wao walishindwa walipoifanya sheria kuwa ya muhimu sana. Walipoteza ufahamu wa kazi ambayo Mungu aliwataka wafanye. Isaya alikuwa amesema kwamba Israeli ilipaswa iwe "nuru kwa watu wa Mataifa." Hii inamaanisha kwamba ilipaswa kushiriki ufahamu wake wa Mungu na watu wengine. Israeli ilipaswa iwe mtumishi ambaye mateso yake yatawafaidi wanadamu wote. Lakini Israeli ilipoteza uwezo wa kuona mwito wake.

Mwishowe, nabii huyu anatumia neno "mtumishi" kuzungumza juu ya mtu atakaycockoa watu wa Mungu. Maneno yaliyoko katika Isaya 53:3-6 yanaeleza kazi ya Yesu Kristo miaka mingi kabla ya kuja kwake. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome vifungu hivi.)

Rumi iliitoka Yerusalemu baada ya miaka mingi kupita. Maandiko ya Agano Jipya yanaeleza hadithi ya yale yaliyotokea.

Weka mkono wako wa kushoto katika mwanzo wa Agano Jipya na mkono wako wa kulia katika sehemu ya mwisho ya Agano Jipya.

Uliza: Je! tunaambiwa nini katika sehemu hii ya Biblia? (Ngojeka majibu.)

Sema: Nitawaambia kwa ufupi kilichoko katika Agano Jipya.

Yohana Mbatizaji nabii wa mwisho wa Kiebrania, alifika na akasema kwamba "Siku ya Hukumu" i karibu. Yesu naye akazaliwa wakati ulipotimia. Malaika walitangaza "Habari Njema" ya kuja kwa Kristo. Agano Jipya inazungumzia kuhusu habari njema za ukombozi wa Mungu jinsi Isaya alivyokuwa amesema kuhusu kuja kwa ukombozi wa Mungu. Mungu alikuwa amefanya "tendo lingine kuu." Tendo hili la Mungu lilibadilisha historia yote. Liko katikati ya imani ya Mkristo.

Ni kilele cha kujifunua kwa Mungu kwa mwanadamu. Yesu Kristo ndiye habari njema. Amekuja kuwaokoa wanadamu na kuwapa maisha mapya.

Katika kitabu cha Kutoka Mungu aliwatoa watu wake kutoka utumwani. Hili lilikuwa tendo kuu la Mungu. Kutolewa kwa Wayahudi kutoka uhamishoni kule Babeli ilikuwa kazi ya Mungu. Sasa Mungu amefanya kazi iliyokuu kushinda zote. Alimtuma Yesu aishi, afe na afufuke. Wanadamu wanaweza kuwa na ushirikiano mpya huu na Mungu na wao kwa wao.

Yesu aliwaita wale wanafunzi kumi na wawili. Mwujiza mkuu ulifanya wakati watu hawa walipoelewa maana ya maisha kufa na kufufuka kwa Yesu. Jamii hii ndogo ilikuwa kanisa. Jamii hii hakupaswa iwe ya watu wachache tu, bali ilikuwa kwa kila mtu, iwapo ni Myahudi au mtu wa Mataifa. Mtu ye yote anaweza kuwa sehemu ya jamii hii, yaani kanisa, iwapo ataamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu na kwamba damu yake ilimwagika kwa ajili ya dhambi zake na akubali kwa imani kufa na kufufuka kwa Yesu, na amkubali Kristo awe Bwana wa maisha yake. Jamii hii, kanisa, ndiyo Israeli mpya. Ni jamii ya Agano Jipya.

Agano Jipya inatwambia kuhusu kazi ya Yesu Kristo katika uanzilishi wa kanisa. Inatwambia pia jinsi Kanisa lilivyoenea katika sehemu mbalimbali za ulimwengu wa siku hizo. Agano Jipya inazo barua (Waraka) nyingi ambazo Paulo na watu wengine waliandikia makanisa mbalimbali.

Sema: Vifungu hivi vya Mathayo 28:16-20 vinatwambia jinsi Yesu alivyolipa kanisa kazi ya kufanya. Mwambie mmoja asome vifungu hivi.

Uliza: Je! kazi ya kanisa ni ipi?

Sema: Ni kushiriki habari njema ya Yesu Kristo na ulimwengu wote.

Uliza: Je! sasa mnaelewa "daraja" inavyounganisha Agano la Kale na Agano Jipya? Mungu aliagana upya na Israeli kupitia kwa Yesu Kristo wakati waliposhindwa kutii agano ambalo Mungu alikuwa amefanya nao.

Uliza: Je! hii inawasaidia kuelewa ni kwa nini sehemu ya kwanza ya Biblia inaitwa Agano la Kale, hali sehemu ya pili inaitwa Agano Jipya?

Sema: Kumbukeni kwamba Mungu alikuwa tu na mpango mmoja, hata ingawa alipaswa kuagana upya na watu wake. Kuna ujumbe mmoja mkuu katika Biblia ambao unaunganisha pamoja Agano la Kale na Agano Jipya. Biblia inazungumzia kuhusu upendo na jinsi Mungu anavyojishughulisha na mwanadamu, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mwishowe, Mungu alidhihirisha wazi mpango wake wa kumwokoa mwanadamu. Mpango huo ulikuwa wa kumrudisha mwanadamu kuweza kushirikiana na Mungu kupitia kwa Yesu Kristo. Yesu hakuja kuanzisha mpango mwingine. Yesu amesema katika Mathayo 5:17 kwamba, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii, la, sikuja kutangua, bali kutimiliza."

Biblia inatwambia jinsi Mungu alivyofanya kazi katika maisha ya mwanadamu ili kumkomboa kila mwanadamu. Mungu yungali anafanya kazi ulimwenguni kupitia

kwa Kanisa lake. Kitabu cha mwisho cha Biblia, UFUNUO, kinasema kwamba Mungu atashinda kabisa wakati wa mwisho.

Kwa muda wa wiki kumi zifuatazo tutajifunza yale ambayo Yesu alisema kuhusu sheria na jinsi alivyoitimiza.

KAZI YA KUFANYA

Katika masomo matatu yaliyopita, tumejifunza jinsi Mungu alivyo-shirikiana kikazi na mwanadamu, jinsi ilivyoandikwa katika Biblia.

Hapo chini kuna sentensi ambazo zinatwambia baadhi ya mambo ambayo Mungu alifanya. Orodha ya mambo haya haijafuatana vizuri. Andika namba kando yake kulingana na jinsi yalivyofanyika.

2 Mungu aliwapa Waisraeli Amri Kumi kupitia kwa mtu aitwaye Musa.

1 Mungu alimwita Ibrahimu na akafanya agano naye. Alimwambia kuondoka katika nchi yake na kwenda katika nchi ambayo atamwonyesha.

4 Mungu aliwaonya watu juu ya matendo yao maovu kupitia kwa watu waitwao manabii.

3 Mungu aliwaongoza Waisraeli hadi Nchi ya Ahadi, Kanaani.

6 Mungu alifanya agano jipya na watu wake. Alimturna Mwanawe Yesu kuja ulimwenguni ili awaokoe wanadamu kutoka katika dhambi zao na kuwa-

rudisha katika ushirika wa haki naye.

5 Mungu aliwatoa Waisraeli kutoka uhamishoni (utumwani) kule Babeli.

7 Yesu Kristo alianzisha kanisa ili kueneza habari njema kwa ulimwengu wote.

Baadhi ya watu hawaelewi nabii ni nani. Jifunze maelezo yafuatayo.

Nabii ... Neno "nabii" katika lugha ya Kiebrania linamaanisha yule anayezungumza kwa niaba ya wengine. Nabii wa Kiebrania aliwaambia watu ujumbe wa Mungu. Wakati mwingine alitoa ujumbe wa matumaini akieleza yale ambayo Mungu atafanya wakati ujao. Nabii alikuwa mtu ambaye alijisikia kuwa ameitwa na Mungu kuhubiri na kuzungumza kwa ujasiri badala yake.

Injili ... Neno hili "Injili" linamaanisha "habari njema". Mafundisho na maisha ya Yesu, hasa kifo chake, kuzikwa na kufufuka kwake, ni injili za Kristo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Sisi sote kama kondoo tumepoten, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:6).

Mungu amekuwa akijishughulisha katika kumrudisha mwanadamu kuwa na ushirika mwema naye tangu wakati

mwanadamu alipofanya dhambi, na kumwasi. Mwishowe, alimtuma Yesu ulimwenguni ili atufie ndipo tusamehewe dhambi zetu.

Kila mmoja wetu amefanya dhambi. Yesu Kristo amefia kila mmoja wetu. Je! unashukuru kwa ajili ya zawadi hii kubwa ya wokovu? Ikiwa unashukuru, basi utaonyesha shukrani zako kulingana na jinsi unavyoishi. Utamkubali kwa imani, na uwe sehemu ya kanisa lake, na ufanye kazi ya kuwaambia wengine yale ambayo Kristo amekufanyia.

WAKATI WA MWISHO

Rudia tena kuzungumzia maana ya Biblia ambayo wanafunzi waliandika katika somo la kwanza. Unaweza kuwaambia waandike maana nyingine iwapo sasa ufahamu wao umebadilika.

Funga kwa maombi ya kumwomba Mungu amsaidie kila mwanafunzi aelewe wajibu wake kama sehemu ya kanisa.

SURA YA NNE

MPENDE MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:3; Mathayo 4:8-10; Marko 12:28-30

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Pengine wengi wao wanajua Amri Kumi zote. Lakini, iwapo hawajui waambie wajifunze kwa moyo. Kutoka 20:3-17.

Pengine wanafunzi hao hawajawahi kufikiria jinsi Yesu alivyofanya amri hizi. Watajua vizuri jinsi ya kutii amri hizi iwapo wataclewa jinsi Yesu alivyofundisha kuhusu amri hizi.

Somo hili ni mwanzo wa mafunzo yahasuyo Amri Kumi. Itakubidi kuhakikisha kwamba unaclewa kila jambo lihusulo amri hizi linalohitajika kutoka kwako kama mwana wa Mungu.

Kutakuwa na Maandiko kutoka katika Agano la Kale na Agano Jipya katika kila somo. Kulingana na vile ilivyoelezwa, twaona kwamba Yesu hakuja kuipinga sheria, bali kuitimiza. Yesu anatupa uelewaji mkuu wa maana ya amri hizi katika mafundisho yake.

Watoto huweza kujifunza vizuri wakati waonapo kitu fulani. Kwa hivyo, andika kila wiki kwenye karatasi na kwa herufi kubwa amri ambayo ni ya wiki hiyo. Ibandike ukutani au kwenye ubao na uiache hapo. Ongezea amri nyingine wiki ifuatayo.

Soma amri ya kwanza kutoka Kutoka 20:3 na mafunzu yale mawili ya Agano Jipya. Mathayo 4:8-10 inatuonyesha kwamba hata Yesu alijaribiwa katika kuabudu miungu mingine. Ibilisi alijua kwamba angeweza kumshinda Yesu iwapo angemfanya asahau sababu iliyomfanya Mungu amtume ulimwenguni. Ibilisi aliahidi kumpa Yesu falme zote za ulimwenguni hata ingawa hazikuwa zake. Yesu alimpinga Ibilisi na akakariri amri ya kwanza.

Mazungumzo ya Yesu na mwandishi katika Marko 12:28-30 yanatuonyesha kwamba aliifikiria amri ya kwanza kuwa ya muhimu sana kwa zote. Mtu hawezi kutii amri zingine iwapo hampendi Mungu kuliko kitu kingine cho chote.

Tilia mkazo ukweli ufuatao wakati unapofundisha:

1. Kitu au mtu ye yote ambaye tunampenda sana na kumpa nafasi ya kwanza maishani mwetu ni "Mungu" wetu.
2. Ni Yehova tu, Mungu wa kweli, ambaye anastahili upendo na heshima yetu.
3. Sisi huweza kutii sheria zingine zote tunapompenda Mungu kuliko kitu kingine cho chote.

KUSUDI LA SOMO HILI:
Kuwaongoza wanafunzi kuweza kutambua baadhi ya miungu ya uongo na kuelewa jinsi wawezavyo kumfanya Mungu kuwa wa kwanza maishani mwao.

KULIFUNDISHA SOMO

Andika ubaoni Kutoka 20:3, au unaweza kubandika ubaoni au ukutani iwapo umeandika kifungu hiki kwenye karatasi.

Uliza: Je! kunaye awezaye kuniambia mahali ambapo kifungu hiki kinapatikana katika Biblia? (Ngojeka majibu.) Waambie wanafunzi hao watafute kifungu hiki katika Biblia zao. Kisomeni wote kwa pamoja.

Sema: Mungu anataka awe wa kwanza miyoni na maishani mwa watu wake. Mungu ndiye alituumba. Anataka kuwa na ushirika nasi. Anatupenda na anatutaka tumpende.

Sema: Amri hii ambayo tumeisha soma ni ya kwanza katika zile Amri Kumi ambazo Mungu alimpa Musa katika Mlima Sinai. Uliza: Kunaye awezaye kutwambia jinsi Mungu alivyowapa watu wake Amri Kumi? (Jadiliana majibu hayo.)

Uliza: Je! mnafikiri kwamba watu wa Mungu walitii kila mara amri hii ya kwanza? La, hawakuitii. Walishindwa kuitii mara kwa mara. Baadhi yao waliabudu muungu wa sanamu aitwaye Baali. Mungu alimtuma mmojawapo wa manabii wake kwao. Nabii huyu, Eliya, aliwakemea watu hao na akawauliza

wataendelea mpaka lini kuwatumika miungu wawili. Eliya aliwaambia kwamba, "Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuateni, bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! mfuateni yeye" (1 Wafalme 18:21).

Uliza: Je! mnafikiri kwamba Eliya alimfahamu Mungu wa kweli? Ndiyo, alijua kwamba Baali hakuwa Mungu, bali sanamu. Bwana ndiye wa kweli, Mungu aishiye ambaye anawapenda watu wake na huwasaidia. Ni Mungu tu wa kweli, aishiye ambaye anaweza kupenda.

Tunajua kwamba Mungu amekuwa akiwapenda watu ambao aliwaumba kwa sababu tunayo rekodi ya upendo wa Mungu kwa watu wake katika Biblia. Tumejifunza kuhusu rekodi hii kwa muda wa wiki tatu zilizopita. Mwanadamu alifanya dhambi. Alikosa kumtii Mungu.

Uliza: Je! Mungu aliacha kutompenda Mwanadamu? Sema: La, Mungu aliendelea kunena na mwanadamu kupitia kwa watu kama Ibrahimu, Musa, Eliya na manabii wote, lakini mwanadamu aliendelea tu kutokuwa na ushirika kati yao. Lakini Mungu alimpenda sana mwanadamu hata akajaribu njia nyingi za kuondoa ukuta ambao ulimtenganisha mwanadamu na Mungu. Mwishowe, Mungu alikuja ulimwenguni katika Yesu Kristo. Yesu anatuonyesha jinsi Mungu alivyo. Anatuonyesha kwamba Mungu ni pendo. Alitufia ili aweze kuondoa ukuta wa dhambi na kutotii kati yetu. Sasa tunaweza kujua upendo wa Mungu iwapo tutampokea maishani mwetu.

Uliza: Je! Yesu alijaribiwa ili afuate njia yake mwenyewe? Ndiyo, Ibilisi alimjaribu Yesu mara tu alipobatzwa. Ibilisi alitaka kuhangaisha Yesu kuhusu kile ambacho Mungu alikuwa amemtuma afanye ulimwenguni na jinsi anageweza kulifanya.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Mathayo 4:8-10. Uliza: "Je! Ibilisi alisemaje alipomwonyesha Yesu milki na falme zote za ulimwengu?"

Uliza: Yesu alimjibuje Ibilisi? (Alimwambia kwamba. "Nenda zako Shetani, kwa maana imeandikwa, 'Msujudi Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake'" (Mathayo 4:10).

Uliza: Je! kifungu hiki ambacho Yesu alitumia kilitoka wapi? Ni kifungu tulichosoma katika Kutoka 20:3.

Uliza: Je! huwa unamjibu ibilisi kwa kutumia Maandiko anapokujaribu kutenda maovu?

Sema: Marko 12:28-30 inatwambia jinsi Yesu alivyoifikiria amri ya kwanza kuwa ya Muhimu.

Wachague wanafunzi wawili wasome vifungu hivi. Mmoja wao atapaswa kusoma maneno ya Yesu na wengine yale ya mwandishi.

Sema: Yesu alikariri fungu la maneno kutoka katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Hebu tutafute kifungu hicho katika Kumbukumbu la Torati 6:4 na 5, na

tukisome pamoja. (Kisomeni wote kwa sauti moja.)

Uliza: Je! inamaanisha nini kumpenda Mungu kwa njia hii? (Wape nafasi ya kuweza kujibu.)


Mungu anawataka watu wake kumpenda yeye kila mara kuliko kitu kingine cho chote. Je! tunampenda zaidi kuliko mtu au kitu kingine cho chote?

Uliza: Huwa tunaonyeshaje kuwa tunampenda Mungu zaidi kuliko mtu au kitu kingine cho chote?

Sema: Tutamruhusu Mungu awe Bwana wa maisha yetu tutakapompenda zaidi kuliko kitu kingine cho chote. Tutataka kumtumikia na kuishi kwa ajili yake kila siku. Huwa tunamtumikia Mungu wakati tunapomtii. Nasi tutamtii iwapo tunampenda.

Uliza: Je! mnafikiri kwamba tunaweza kutii amri zingine iwapo tutashindwa kumpenda Mungu zaidi kuliko mtu au kitu kingine cho chote? La! Hatuwezi kuishi maisha ya haki bila msaada wa Mungu. Tutapata nguvu za kushinda majaribu na dhambi tutakapomruhusu Mungu kuishi maisha yake ndani yetu. Pia, tutapata ushindi maishani wakati tutakapomruhusu Roho wake kutuongoza.

Waeleze kuhusu sehemu ya "Kazi ya Kufanya" na usahihi majibu yao wakati watakapo maliza kazi hiyo.



KAZI YA KUFANYA

Hapa kuna picha ya mbao za mawe inayofanana na ile iliyoandikwa zile Amri Kumi. Andika amri ya kwanza kwenye picha hii. (Tazama Kutoka 20:3.)

Kuna maneno ambayo yameachwa katika aya ifuatayo. Utapata maneno na picha inayoelezea katika orodha iliyoko chini ya sentensi hizi. Jaza nafasi ilioachwa kwa neno lililosahihi.

Mungu aliwataka watu wake wampende sana kila wakati, lakini hawakufanya hivyo wakati wote. Wakati mmoja waliabudu SANAMU mkubwa aitwaye Baali. Hata siku hizi kunao watu wengine ambao wanapenda sana mali na vitu vingine zaidi kuliko Mungu. Baadhi ya watu wanapenda sana PESA zaidi kuliko kitu kingine. Au wanaweza kufikiri kwamba utajiri unapatikana kwa

kuwa na NG'OMBE, na ni wa muhimu sana. Watu wengine hufanya ELIMU kuwa ya kwanza maishani mwao. Watu wengine hufikiria kwanza vitu kama GARI nzuri. Wengi hufanya nafsi yao kuwa ya kwanza, wakitaka tu kujifurahisha bila kuwafikiria wenzao.



Ng'ombe



pesa



gari



sanamu

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“...Ya kwanza ndiyo hii, sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote” (Marko 12:29-30).

Mwandishi mmoja alimwendea Yesu na akamwuliza ni amri ipi iliyo ya kwanza kwa zote. Yesu alimjibu kwa kumwambia maneno yaliyo katika kifungu cha kukumbuka cha leo. Hatuwezi kuwapenda wenzetu iwapo hatumfanyi Mungu kuwa wa kwanza na pia kumpenda sana. Hatuwezi kuishi jinsi inavyotupasa iwapo hatutii amri hii ya kwanza.

WAKATI WA MWISHO

Jaribu kulinganisha amri hii na maisha ya wanafunzi wako. Waambie wataje vitu ambao vijana wa umri wao hupenda sana kuliko Mungu.

Waambie sasa wainamishe vichwa vyao. Baada ya kuinamisha, waambie wamwombe Mungu awaonyeshe njia moja ambayo wataweza kumfanya awe wa kwanza maishani mwao. Funga kwa maombi ukimwomba Mungu awawezesha kumfanya awe wa kwanza maishani mwao.

Watie moyo wanafunzi hao ili waweze kujifunza Kutoka 20:3 kabla ya wiki ijayo.



elimu

Utataka kumtii Mungu iwapo unampenda. Andika katika nafasi ifuatayo njia moja wapo ambayo utajaribu kumtii Mungu kwayo wiki hii ijayo.

SURA YA TANO

MUNGU ANATAKA IBADA YA KWELI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:4-6; Yohana 4:7-10, 19-24.

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Ukweli ambao utasisitiza unapofundisha leo, ni lazima utegemea hitaji la wanafunzi wako. Pengine watoto walioko katika darasa lako wanaishi katika eneo ambalo kuna utumiaji mwingi wa hirizi, sanamu na uchawi. Pengine wamejifunza kutoka kwa wazazi wao umuhimu wa ukoo katika mila na desturi zao. Ikiwa wanaamini hivi, basi utapaswa kudhihirisha wazi amri ya Mungu kuhusu utumiaji, kuamini, au kuabudu kitu kingine badala ya Mungu wa kweli.

Pengine wanafunzi wa darasa lako hawatakuwa na ufahamu mzuri juu ya mambo haya. Hata hivyo, utapaswa kutilia mkazo maana ya ibada ya kweli na jinsi tuwezavyo kumwabudu Mungu vyema.

Amri ya pili ni karibu sawa na ile ya kwanza. Amri zote zinafundisha kwamba ni lazima Mungu awe wa kwanza maishari mwa Mkristo.

Andika kwenye karatasi sehemu ya kwanza ya amri ya pili. "Usijifanyie sanamu ya kuchonga" (Kutoka 20:4a). Bandika karatasi hii ubaoni au ukutani karibu na ile ya kwanza uliyotumia wiki iliyopita wakati unapofundisha.

Kuna mafungu mengine katika Biblia ambayo yanafundisha ukweli uliosawa na amri ya pili. Utapaswa

kusoma mafungu yafuatayo: Isaya 44:9-20; Kumbukumbu la Torati 7:25-26; Mambo ya Walawi 26:1-2. Sasa soma yale ambayo Yesu alisema kuhusu ibada ya kweli alipokutana na mwanamke Msamaria. (Yohana 4:7-10, 19-24).

Tilia mkazo ukweli ufuatao wakati unapofundisha:

1. Amri ya pili ambayo Mungu aliwapa watu wake iliwaambia kutofanyikiza au kuabudu mfano wa kitu cho chote.
2. Mungu anawataka watu ake wamwabudu yeye tu.
3. Yesu alisema kwamba ni lazima tumwabudu Mungu kwa roho na kweli.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kuelewa maana ya ibada ya kweli ili uelewaji wao uwasaidie katika kuabudu kwao.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! kunaye awezaye kukariri amri ya kwanza? Sasa, kunaye awezaye kusema amri ya pili bila kusoma?

Bandika ubaoni au ukutani karatasi uliyoandika amri ya pili baada ya kusikiliza majibu yao. Ibandike chini ya karatasi uliyoandika amri ya kwanza.

Sema: Amri ya kwanza ya Mungu ilisema kwamba hatupaswi kuwa na miungu mingine ila Mungu wa kweli.

Tulijifunza amri hii wiki iliyopita. Leo twaona kutoka kwa amri ya pili kwamba Mungu hataki watu wake waabudu sanamu au mfano wa wote. Anawataka wampende na wamwabudu yeye tu. Yeye ndiye Mungu wa kweli aishiye.

Uliza: Je! "sanamu ya kuchonga" ni nini?

Sema: Sanamu ya kuchoma ni kama mfano wa kitu cho chote. Ni kitu kilichotengenezwa na mwanadamu kutoka kwa mbao, jiwe au chuma.

Uliza: Je! ibada ni nini? (Wanafunzi wanaweza kutoa majibu kama haya: ni sifa, shukrani, kuimba, maombi. Andika majibu hayo ubaoni iwapo unao.)

Sema: Ndiyo, ibada ni pamoja na mambo haya yote, lakini ni zaidi ya hayo. Ibada ni yale tusemayo na tunayosikia moyoni mwetu. Ibada ni kuonyesha jinsi Mungu alivyo wa ajabu. Ni mwenye upendo kwa sababu alituma Mwanawe kufa kwa ajili yetu. Yeye ni mkarimu, kwa sababu anatumiza kila siku. Mungu anatumiza tumwabudu. Ibada si kumwambia tu Mungu, "Asante" kwa vyote anavyokupatia, bali ni kusema tunampenda kwa jinsi alivyo.

Uliza: Je! kunayo njia nyingine yeye yote ambayo tunaweza kuabudu? (Ngoja majibu.)

Sema: Ndiyo, ibada ni zaidi ya kushukuru na kuimba nyimbo za sifa. Ikiwa kweli tunamwabudu Mungu basi tutaishi kwa njia ambayo

itampendeza. Tunamwabudu Mungu kwa matendo yetu na nia zetu. Maombi na kuimba kwetu kuna faida ndogo sana iwapo mambo tufanyayo na kufikiria kila siku hayampendezi Mungu.

Sema: Siku moja Yesu alizungumza na mwanamke Msamaria juu ya kuabudu. (Mchague mwanafunzi mmoja asome Yohana 4:7-10 na 19-24.)

Sema: Mwanamke huyu alitaka kujua mahali pazuri pa kumwabudia Mungu.

Uliza: Yesu alimwambiaje? Alimwambia kwamba mahali pa kuabudia si pa muhimu. Ni muhimu jinsi mtu anavyoabudu. Ni lazima tumwabudu Mungu "katika roho na kweli". (Jadiliana maana ya jambo hili. Waambie kwamba Mungu ni roho na hawezi kuwakilishwa na kifaa cho chote.)

"Katika kweli" inamaanisha kwamba ni lazima tufanye kwa nia ya moyo na haki.

Uliza: Tunawezaje kufanya yale ambayo Yesu alisema?

Sema: Ni lazima tuwe na mioyo ya haki na misafi mbele za Mungu kabla ya kumwabudu. Mwanamke Msamaria alikuwa mwenye dhambi sana. Alianza kutambua kwamba ni lazima asamehewe. Hakujua mahali pa kwenda ili akutane na Mungu. Yesu alimsaidia kuelewa kwamba alikuwa Mwokozi ambaye Mungu alikuwa amehidi kwamba atamtuma. Alikuwa tayari kuabudu baada ya

kumkubali Yesu kama Mwana wa Mungu.

Wasaidie wanafunzi na sehemu ya “Kazi ya Kufanya” na ueleze maana ya kifungu cha kukumbuka.

KAZI YA KUFANYA

Kuna sentensi hapo chini. Baadhi yazo zinaelezea matendo ya ibada ya kweli, na zingine hazielezei. Andika neno NDIYO kando ya sentensi zielezayo ibada ya kweli na uandike LA kando ya zile zingine.

NDIYO 1. Nazitazama nyota na kusema, “Mungu ni wa ajabu. Aliumba ulimwengu na vyote vilivyomo. Hali yungali na muda wa kunisikiliza.”

LA 2. Kuna sanamu moja ya mwanadamu kwenye meza pale ukutani. Mtu mmoja huisujudia na kuweka chakula karibu nayo.

LA 3. Samweli hufunga macho yake wakati mchungaji anapoomba, lakini huwa anafikiria mchezo wa mpira aliocheza wiki iliyopita.

LA 4. Mariamu huwa anasema kwa haraka sala alilokariri kabla ya kulala na kuitikia “Amina”, halafu anachukua kitabu cha hadithi na kuanza kukisoma.

NDIYO 5. Wanjiru humwangalia mtoto na kusema, “Ona mtoto huyu alivyomzuri! Hebu

viangalie vidole vyake. Ni ajabu ilioje jinsi Mungu alivyofanya muumbo wa kupendeza?”

Taja mahali patatu ambapo unaweza kumfanyia Mungu ibada ya kweli.

1. _____
2. _____
3. _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Mungu ni roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli” (Yohana 4:24).

Tunapomwabudu Mungu tunapaswa kukumbuka yale aliyosema Yesu. Mungu ni roho. Yuko kila mahali. Hatuwezi kumwona lakini yu pamoja nasi tunapoabudu. Tunaweza kumwabudu Mungu wakati wote na mahali po pote kwa sababu yeye ni roho. Ibada yetu huwa inakubaliwa iwapo yale tunayosema na kufanya wakati wa ibada ni ya kweli.

Hatupaswi kutumia sanamu wakati wa ibada kwa sababu Mungu ni roho. Biblia inatwambia kwamba Mungu yu ndani yetu iwapo sisi ni Wakristo. “Hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu?” (1 Wakorintho 6:19). Mungu yu nasi kila mara kwa sababu anaishi ndani yenu. Kwa nini tuhitaji msaada wa sanamu hii tumfikirie Mungu? Jambo hili halimpendezi Mungu?

WAKATI WA MWISHO

Waongoze wanafunzi hao katika kusoma Zaburi 45:1-7 iliyo kwenye ukurasa ufuatao. Wahimiza ili waweze kujifunza zaburi hii wiki ijayo.

Mwambie kila mwanafunzi ambaye atajifunza zaburi hii aombe kwa maneno mafupi akionyesha sifa na shukrani zake kwa Mungu.

Njoni, tumwimbie Bwana, tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu. Tuje mbele zake kwa shukrani, tumfanyie shangwe kwa zaburi.

Kwa kuwa Bwana ni Mungu mkuu, na mfalme mkuu juu ya miungu yote.

Mkononi mwake zimo bonde za dunia, hata vilele vya milima ni vyake.

Bahari ni yake, ndiye aliyeifanya, na mikono yake aliumba nchi kavu.

Njoni, tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba.

Kwa maana ndiye Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake, na kondoo za mkono wake."

Zaburi 95:1-7a

UWE MWAMINIFU KATIKA IBADA

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:7; Mathayo 5:33-37; Marko 7:5-8

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Pengine hawatajua unachomaanisha unaposema kwamba, "Usilitaje bure jina la Bwana." Utakazia kwamba kutokuwa mtiifu katika ibada ni njia mojawapo ya kulitaja bure jina la Bwana. Unapaswa pia kuwasaidia waelewe kwamba ni muhimu jinsi wanavyotumia jina la Mungu katika maongezi yao. Baadhi ya wanafunzi waliojifunza kizungu kama lugha ya pili au ya tatu hawawezi kutambua baadhi ya usemi ambao haufai katika mazungumzo ya Mkristo. Uwe tayari kujadili mambo haya na wanafunzi wako.

Amri ya tatu inasema kwamba, "Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako, maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure" (Kutoka 20:7). Amri hii inatwambia tusitumie vibaya jina la Mungu. Yesu alituonya juu ya kuapa. Utapaswa kusesitiza fundisho hili, lakini usiachie tu hapo. Amri hii inamaanisha zaidi ya hapo. Inamaanisha pia kwamba hatupaswi kutumia jina la Mungu bila nia nzuri katika ibada.

Soma Luke 18:11-12 pamoja na Maandiko uliyopewa hapo juu. Unapata mfano mzuri hapa wa mtu, Mfarisayo, ambaye alimheshimu Mungu kwa mdomo wake, hali moyo wake ulikuwa mbali sana na Mungu.

Fungu hili halijatumiwa katika kitabu cha wanafunzi, lakini unaweza kulitumia wakati unapofundisha. Pengine utawataka wanafunzi waige mchezo wa hadithi hii. Jambo hilo hilo limesisitizwa katika Marko 7:5-8 ambapo Yesu anawaambia Mafarisayo kwamba wamefanya sheria za wanadamu kuwa za muhimu zaidi kuliko kumheshimu Mungu.

Vifungu vya Mathayo 5:33-37 vinatupa fundisho la Yesu kuhusu kuapa.

Andika amri hiyo ya tatu kwenye karatasi jinsi ulivyoandika zile zingine: "Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako."

Hebu chunguza maisha yao wenyewe. Jiulize hivi, "Je! ibada yangu ni ya kweli? Je! huwa ninasema maneno ya sifa kwa mdomo tu ambapo hayapo ndani ya moyo wangu? Je! ninajihadhari na mazungumzo yangu ili nisilitaje bure jina la Mungu?"

Tilia mkazo mambo yafuatayo wakati unapofundisha:

1. Amri ya tatu ambayo Mungu aliwapa watu wake iliwaambia kwamba wasilitaje bure jina lake.
2. Yesu alisema kwamba watu walizungumza kama kwamba wanampenda Mungu, lakini mioyo yao ilikuwa mbali sana naye.

3. Yesu alipinga kutumia vibaya jina la Mungu.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwaongoza wanafunzi katika kuchunguza maisha yao na mazungumzo yao na waone iwapo wanalitaja bure jina la Mungu.

KULIFUNDISHA SOMO

Sema: Je! huwa mnaimba wimbo huu usemao, "Nakupenda, mama?" Unasimulia hadithi ya watoto watatu. Walianza siku kwa kumwambia mama yao kwamba wanampenda. Yohana, ambaye ni mdogo kwa wote, ndiye aliyesema kwanza, "Nakupenda." Halafu akaenda nje kucheza. Hakufanya kazi ambayo mama yake alimwambia afanye. Hatimaye, dada yake aitwaye Anna akasema, "Nakupenda." Lakini alikaa tu akiwa amenung'unika na hata akamkasirisha mama yake. Mama huyo alifurahi sana wakati Anna alitoka nje na kwenda kucheza. Mtoto mwingine aitwaye Mariamu akasema, "Nakupenda" na akaonyesha upendo wake siku nzima. Alisaidia katika kumtunza mtoto na kufagia nyumba. Alikuwa akiimba na kuonyesha furaha alipofanya kazi hiyo. Mwishowe wimbo huu unauliza swali hili, "Je! unafikiri mama huyu alijuaje yule mtoto ambaye anampenda sana?"

Uliza: Je! mnafikiri mama huyu alijuaje yule anayependa sana? Mungu atajuaje iwapo unampenda au unasema tu hivyo?

Bandika amri ya tatu ubaoni au ukutani.

Uliza: Je! mnafikiri amri hii inamaanisha nini? (Ngojea majibu.) Mwambie mmoja wao asome Mathayo 5:33-37.

Sema: Yesu alisema kwamba, "Usiape kabisa." Je! huwa unaapa? Je! kuapa ni nini? Kuapa ni kutumia jina la Baba wa Mbinguni au jina la Mwanawe, Yesu, wakati ambapo hatunuiwi kamwe kuzungumza na Mungu.

Sema: Ni bivaya kutumia jina la Mungu ili kusisitizia yale usemayo. Huwa tunafanya hivyo wakati tusemapo maneno kama, "Haki ya Mungu, nilisahau." au "Mungu anajua tu nasema ukweli." Hatupaswi kutumia jina la Mungu tunapoapa au kulaani. Jina la Mungu ni takatifu jinsi yeye mwenyewe alivyomtakatifu. (Wape muda wa kujadiliana.)

Sema: Maana ya amri ya tatu ni zaidi ya yale tunayosema tu. Inamaanisha pia jinsi tunavyoishi. Iwapo tunasema kwamba tunamjua Mungu, hali tunaishi kama hatumjui, basi, tunaivunja amri hii.

Uliza: Je! mnafiki ni nani? (Wape wanafunzi hao muda wa kutafuta jibu lake katika somo lao na walijadili.)

Sema: Hebu tusome Marko 7:5-8. Watu walioelezwa hapa ni wanafiki. (Soma Marko 7:5-8 au mchague mwanafunzi mmoja asome.)

(Sasa simulia hadithi ya Mfarisayo na mtoza ushuru wakati unapo-waonyesha picha hiyo au uwaambie wanafunzi waiangalie katika vitabu vyao. Hadithi hii inapatikana katika

Luka 18:9-14. Picha yenyewe inapatikana katika ukurasa wa mwisho wa somo hili.

Sema: Watu hawa walioko katika picha hii wako hekaluni, mahali ambapo watu walienda kumwabudia Mungu. Mtu aliyeko katika upande wa kushoto anajifanya kuwa anaabudu. Pengine alileta sadaka fulani jinsi watu wengi wafanyavyo. Tunaposoma maneno aliyomwambia Mungu tunaona kwamba hakuwa akiabudu. Alikuwa akimwambia Mungu jinsi alivyo mtu mwema.

Uliza: Mtu huyu alisemaje? (Mwambie mwanafunzi mmoja asome Luka 18:11-12.)

Sema: Hebu mwangalie yule mtu mwingine aliyeko katika picha hiyo. Ameinamisha kichwa chake. Biblia inasema kwamba alijipiga-piga kifua chake kama kwamba anajiadhibu. Alikuwa akifikiria jinsi Mungu alivyo mkuu na mtakatifu. Utakatifu wa Mungu ulimfanya ajione kuwa mwenye dhambi. Soma maneno yake katika Luka 18:13.

Sema: Mungu alikuwa akiangalia mioyo ya watu hawa wawili. Alijua ni upi uliokuwa unasema tu maneno ili watu wengine wafikirie kwamba alikuwa mtu mwema. Alijua ni mtu aliyekuwa akimfikiria Mungu na jinsi alivyo mwema.

Uliza: Je! unafikiri Mungu alisikia ombi lipi? Ndiyo, ombi la mtoza ushuru. Yule mtu mwingine hakuwa akiomba kamwe.

Sema: Hadithi ya watu hawa wawili haikuwa tu ya watu waliokuwepo

wakati wa Agano Jipya. Inahusu hata sisi pia. Mungu hatutaki tuombe tu ili tuwafanye watu wengine wafikirie kwamba tu wema. Tunapomba tunapaswa kuzungumza na Mungu kutoka mioyoni mwetu na tumaanisha kweli kile tusemacho. Mungu amesema kwamba, "Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo, maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo" (1 Samweli 16:7).

Wasaidie wanafunzi na sehemu ya "Kazi ya Kufanya" na uwaelezee maana ya kifungu cha kukumbuka.

KAZI YA KUFANYA

Sentensi zifuatazo zimetolewa katika Maandiko ya Biblia ya somo la leo. Wameacha nje baadhi ya maneno. Jaza nafasi zilizoachwa kwa kutumia maneno yaliyoko upande wa kushoto. Chagua neno ambalo litakamilisha vyema kila sentensi.

- | | |
|--------------|---|
| huniheshimu | 1. "Lakini mimi nawa-ambia <u>usiape</u> kabisa." |
| jina | 2. "Nao <u>waniabudu</u> bure." |
| maneno | 3. "Bali <u>maneno</u> yenu yawe 'ndiyo' au 'sivyo'." |
| amri | 4. "Usilitaje bure <u>jina</u> la Bwana, Mungu wako." |
| waniabudu | 5. "Watu hawa <u>huni-heshimu</u> kwa midomo yao, ili <u>mioyo</u> yao iko mbali nami." |
| mapokeo | |
| usiape mioyo | 6. "Ninyi mwaiacha <u>amri</u> ya Mungu na kuyashika <u>mapokeo</u> ya wana damu." |

Hebu jifikirie wewe mwenyewe. Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika "Ndiyo" au "la".

Je! huwa unasema kwa mdomo wako kwamba, "Nampenda Mungu?"

Je! huwa unasema maneno haya kwa moyo wa kweli? _____

Je! huwa unasoma na kuisikiliza Biblia? _____

Je! matendo yako huwa yanadhahirisha maneno yako? _____

Je! huwa unamwomba Mungu akusaidie uishi maisha ya kumpendeza? _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Na kwa nini mnanita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi niemayo?" (Luka 6:46).

Kusema tu, "Bwana, Bwana," haikumaanisha cho chote iwapo hatumfuati Mungu daima. Watu wengi siku hizi wanaweza kusema kwamba, "Ndiyo namwamini Mungu." Hali maisha yao yanaonyesha kwamba hawamjali Mungu kamwe. Kutenda hivi ni sawa na kulitaja bure jina la Mungu.

Wafuasi wa Yesu waliitwa Wakristo kwa sababu walikuwa kama Kristo. Huwa tunaabudu bure jina la Mungu iwapo hatuishi jinsi alivyotuagiza tuishi.

WAKATI WA MWISHO

Rudia maana ya kulitaja bure jina la Mungu. Wakumbushe wanafunzi kwamba hatupaswi kulitaja bure jina la Mungu ila tu wakati tunapomfikiria na tunasema kwa kweli yale tusemayo.

Funga kwa maombi.



MATUMIZI MEMA YA SABATO

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 28:8-11; Luka 6:6-11

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! umewatia moyo wanafunzi wako kujifunza kwa moyo amri moja kila wiki. Iwapo hujafanya hivyo, basi anza sasa.

Amri za kwanza nne kati ya zile Amri Kumi ambazo Mungu aliwapa watu wake zinahusu ushirika wa mwanadamu na Mungu. Amri ya nne inasema kwamba, "Ikumbuke siku ya sabato uitakase," (Kutoka 20:8) Je! amri hii ina maana gani kwako kama mtu mzima? Je! unafikiri inamaanisha nini kwa wanafunzi wako? Je! wanaitiije siku ya Bwana? Fikiria majibu ya maswali haya unapojiandaa kufundisha.

Kuna ukweli mwingi ambao unapaswa kufahamu kuhusu siku ya sabato. Kwanza kabisa, Mungu alimpa mwanadamu amri hii tangu mwanzo wa muumbo. Kitabu cha Mwanzo kinatwambia kwamba Mungu aliuumba ulimwengu kwa muda wa siku sita na akapumzika siku ya saba. Neno hili sabato linamaanisha, "Kupumzika au kutofanya kazi." Pili, Jumapili au siku ya Bwana ndiyo sabato ya Wakristo wengi. Wakristo wa mwanzo waliifanya siku ya kwanza ya wiki kama siku iliyotengwa ya kupumzika na kuabudu. Walibadilisha siku ya sabato kutoka Jumamosi hadi Jumapili kama njia ya kukumbuka

kufufuka kwa Yesu. Tatu, Wayahudi walifanyia amri nyingi sana zihusuzo sabato hadi ikawa mzigo mzito kwao kuitakasa siku hii. Siku hii haikukusudiwa na Mungu kuwa mzigo kwa mwanadamu. Ilipaswa iwe siku ya kupumzika na kufurahi. Yesu alikuwa akifikiria kwanza faida ya mwanadamu katika siku hii. Nne, kuna mengi zaidi yanayohusu amri hii kuliko kupumzika siku yote. Sheria hii ni amri ya kufanya kazi kwa siku sita na kupumzika siku moja. Biblia inafundisha kwamba kila mmoja anapaswa kufanya kazi.

Soma Kutoka 20:8-11. Sasa soma Luka 6:6-11. Wayahudi walikuwa wameifafanua vibaya amri hii ya nne. Waliandika orodha ndefu ya mambo ambayo hawangefanya wakati wa siku ya sabato. Hata hawangeweza kumsaidia mtu aliyehitaji msaada. Yesu alisema kwamba walikosa kuelewa maana ya amri hii.

Andika amri ya nne kwenye karatasi jinsi ulivyoandika zile zingine.

Tilia mkazo ukweli ufuatao unapofundisha.

1. Sisi huitakasa siku ya sabato tunapoitumia kwa kuabudu, kupumzika na kuwatendea mema wenzetu.
2. Yesu aliwaponya watu na akatenda mema wakati wa sabato.
3. Wakristo wa mwanzo walikutana siku ya Jumapili ili wamwabudu

Mungu. Waliita Jumapili Siku ya Bwana kwa sababu Yesu alifufuka kutoka kwa wafu siku hiyo.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwaongoza wanafunzi katika kurudia amri nne za kwanza na kuwasaidia kutambua jinsi wawezavyo kuitakasa Siku ya Bwana.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! sheria ya Mungu ya nne kwa watu wake ni ipi? (Ngojea majibu, halafu waonyeshe karatasi ambayo umcandika amri ya nne.)

Uliza: Je! huwa unafanya nini wakati wa Jumapili? (Ngojea majibu). Je! mnafikiri hizo ni njia nzuri za kuitakasa siku hii ya Sabato? (Jadiliana)

Sema: Siku ya sabato, kulingana na wakati wa Agano la Kale, ilikuwa Jumamosi, yaani siku ya saba ya wiki. Wayahudi wote ambao wangali hawajamwamini Yesu, wangali wanaiheshimu Jumamosi kama siku yao ya sabato.

Uliza: Je! mnajua mtu ye yote ambaye angali anaitakasa Jumamosi kama siku ya sabato? (Jadiliana)

Sema: Yesu alifufuka kutoka kwa wafu katika siku ya kwanza ya wiki, Jumapili. Wakristo walianza kukutana wakati wa siku hii badala ya Jumamosi, baada ya Yesu kwenda mbinguni. Wakaanza kuiita, "Siku ya Bwana."

Sema: Wakristo wengi wamecendelea kukutana na kuabudu katika siku hii

ya Bwana, yaani Jumapili. Mungu ametuamuru tuitakase siku hii.

Uliza: Mnafikiri tunawezaje kuitakasa siku hii? (Ngojea majibu.)

Sema: Tunapaswa tuwe waaminifu katika kuhudhuria ibada ya kanisa letu. Tulipewa siku hii kama siku ya kutafuta msaada wa mahitaji yetu ya kiroho.

Sema: Siku ya sabato inapaswa iwe siku ya kupumzika kutokana na kazi tunayofanya kila siku. Tulipewa kama siku ya kupumzika na kupumzisha miili na akili zetu. Mungu hakumaanisha kwamba hatupaswi kufanya cho chote.

Uliza: Je! ni kazi zipi ambazo ni lazima zifanywe siku ya Jumapili? (Jadili majibu hayo). Sema: Ni lazima tupike nyumbani mwetu na tuitunze jamaa. Baadhi ya watu kama madaktari na wauguzi wana kazi ambazo ni lazima wafanye siku ya Jumapili. Mungu analeta jambo hili. Hata hivyo, tunapaswa kuitumia Jumapili kama siku ya kupumzisha miili yetu.

Uliza: Je! huwa unafanya nini wakati wa Jumapili? (Jadili)

Uliza: Je! jamaa yako hungojea kwenda sokoni wakati wa Jumapili badala ya Jumamosi? Huwa unasema kwamba, "Leo siwezi kwenda kuabudu pamoja na Wakristo wengine kwa sababu mama yangu ananitaka niende naye sokoni." Tunapaswa kufanya matayarisho ya Jumapili wakati wa Jumamosi.

Uliza: Je! jamaa yako hufanya nini wakati wa Jumamosi ili kujitayarisha kwa ajili ya Jumapili? (Ngojea majibu.)

Sema: Tunaweza kupata msaada wa jinsi ya kuitakasa siku ya sabato tukifuata mfano na mafundisho ya Yesu. Wayahudi walikuwa na sheria nyingi sana zihusuzo sabato wakati Yesu alipoishi hapa duniani. Kulikuwepo na zaidi ya mambo elfu moja ambayo hawangeweza kufanya wakati wa siku ya sabato. Walikuwa waangalifu sana kuhakikisha kwamba kila mmoja alitii sheria hizi. Wale ambao hawakutii sheria za siku ya sabato waliadhibiwa vikali.

Sema: Hebu tusome hadithi kutoka kwa Biblia ambayo inatwambia kile ambacho Yesu alifanya wakati wa sabato. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome Luka 6:6-11.)

Wape watoto hao nafasi ya kuuliza maswali. Tilia mkazo mafundisho yahusuyo sabato ambayo unadhani wanafunzi wako wanapaswa kujua. Wasaidie katika sehemu ya "Kazi ya Kufanya" ambayo ni marudio ya amri hii ambayo wamejifunza. Waongoze wanafunzi hao katika kurudia kusema amri nne za kwanza.

KAZI YA KUFANYA

Baadhi ya maneno yameachwa katika sentensi zifuatazo. Jaza nafasi zilizoachwa kwa maneno yaliyo sahihi.

1. Musa alipewa Amri Kumi na Mungu kwa ajili ya watu wa kale na wa sasa. Amri hizi zinapatikana katika kitabu cha KUTOKA, sura ya ISHIRINI.

2. Amri ya kwanza inasema kwamba, "Usiwe na MIUNGU mingine ila mimi."
3. Amri ya pili inasema kwamba, "Usijifanyie sanamu ya kuchonga."
4. Amri ya tatu inasema kwamba, "Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu Wako."
5. Amri ya nne inasema kwamba, "Ikumbuke siku ya sabato uitakase."

Hapo chini kuna mchezo unaofanana na fumbo. Hii ni picha ya mtu. Unganisha kila namba jinsi zinavyofuatana kwa kuchora mstari ukianza na namba 1. Utakapomaliza utapata picha ya mtu. Je! mtu huyo ni nani? (Ni Musa, alipokuwa akipewa sheria na Mungu.)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"...Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato. Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato pia" (Marko 2:27 na 28).

Yesu alikuwa akiwaambia mafarisayo kwamba sabato ilitolewa kwa ajili yetu. Hatuhitaji sheria nyingi ili tuitakase Siku ya Bwana. Tunapaswa kujifunza neno la Mungu, tuzungumze naye, na tuabudu na kuomba pamoja na Wakristo wengine. Tunapaswa kupumzisha akili na miili yetu. Tunapaswa kuwatendea wenzetu mema.

WAKATI WA MWISHO


Tumejifunza kuhusu amri nne za kwanza kwa muda wa wiki nne

zilizopita. Amri hizi zote zinahusu ushirika wetu na Mungu. Tumejifunza kwamba Mungu anataka nafasi ya kwanza maishani mwetu. Anatwambia kwamba hatupaswi kusujudia sanamu wala kulitaja bure jina lake. Tunapaswa kuitakasa Jumapili, ambayo ni siku yake.

Wakristo wanapaswa kutii sheria hizi kwa sababu ya upendo wao kwa

Mungu. Tumesoma kwamba Yesu alisema kuwa amri iliyo kuu kwa zote ni kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote, na kwa roho yetu yote na kwa akili zetu zote (Mathayo 22:37). Tutakuwa tumetii amri hizi tulizojifunza iwapo tutafanya hivyo.

Omba kwamba tuweze kumpenda Mungu zaidi kuliko mtu mwengine ye yote au kitu kingine cho chote.



WAHESHIMU WAZAZI WAKO

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:12; Marko 7:9-13; Luka 2:51-52

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Una kazi muhimu sana kama mwalimu katika kanisa lako. Jambo moja linalofanya kazi hii kuwa ya muhimu ni wakati mwingine kuonekana ngumu ni sababu ya mabadiliko yanayofanyika hapa Afrika.

Bila shaka, kulikuwepo na mila (desturi) na sheria nyingi zilizoongoza maisha yako ulipokuwa mtoto kwa sababu ulikuwa ukiishi katika kundi la kabila lako. Lakini siku hizi watu wanahamia sana mijini hapa Afrika. Hawaruhusu kuongozwa maishani wala kutawaliwa na sheria au desturi za kikabila. Watu wengi kati ya hawa si Wakristo, kwa hivyo hawana mafundisho ya Biblia na Yesu ambayo yanaweza kuwaongoza. Watu hawa ni kama kondoo wasio na mchungaji. Waalimu wa Kikristo wana wajibu wa kufundisha msingi wa Biblia uhusio tabia. Watu wengi watageukia njia mbaya za maisha ambazo zitawaangamiza wao na taifa lao iwapo waalimu hawa watashindwa kutekeleza wajibu wao.

Jamaa iko katika hali ya mabadiliko katika kila nchi ya ulimwengu. Amri ya nne imekuwa ya muhimu sana, lakini inawahusu hawa watoto. Pengine wazazi wao wanawaambia wawe watiifu, lakini hawajawahi kuelewa kwamba hii ni amri ya Mungu pia.

Baadhi ya watoto wanaweza kuwa na wazazi ambao si Wakristo. Wengine wanaweza kuwa na wazazi ambao si wapole na hawaonyeshi wanao upendo. Ikiwa hii ni kweli, basi utapaswa kutumia muda mwingi kwa kuwasaidia watoto hawa kuelewa kwamba ni vizuri kuwaheshimu wazazi wao. Mungu atawasaidia hata ingawa wanafikiria hawapaswi kuheshimiwa, kwa sababu ameamuru kwamba wawaheshimu wazazi wao.

Jamaa ambayo watoto wake wanaheshimu na kuwatii wazazi wao huwa jamaa imara. Taifa linapaswa kuwa na jamaa imara ili liendelee kuwa taifa lenye nguvu. Matatizo huwa katika kila taifa wakati jamaa yake huanza kuwa dhaifu.

Mwombe Mungu akuongoze ili uweze kuelewa jinsi hali ilivyo katika kila jamaa ya wanafunzi wako wakati unapotayarisha somo hili. Je! umewahi kutembelea kila jamaa?

Amri nne za kwanza za Mungu zinawaambia watu wake jinsi ya kumtendea, kumwabudu yeye pekee, kulitakasa jina lake na kuitakasa siku yake. Amri zake sita za mwisho zinatuambia jinsi ya kuwatendea watu wengine. Ya kwanza kati ya hizi ndiyo kiini cha somo letu la leo; "Waheshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako" (Kutoka 20:12).

Mungu alikuwa akinena na wana wa Israeli. Alikuwa akiwaonyesha njia

ya kuwa na taifa imara na kuendelea kutenda mema katika nchi ambayo walikuwa wamepewa na Mungu.

Yesu aliifikiriaje amri hii? Mafarisayo waliwalaumu wanafunzi wa Yesu kwa sababu wakati mwingine hawakunawa mikono yao kabla ya kula chakula. Yesu aliwaambia kwamba wao walikuwa na hatia ya kosa kubwa zaidi ya hilo. Wengi wao hawakutaka kuwasaidia wazazi wao waliozeeka. Walisingizia kwamba zawadi ambazo wangewapa wazazi wao, walikuwa wamezitenga kama zawadi za kumtolia Mungu. Hazingetumiwa kwa kuwasaidia wazazi wenye mahitaji. Kwa kweli, Mafarisayo hawa walikuwa wakidanganya ili kuepuka wajibu wao wa kuwasaidia wazazi wao.

Yesu alikuwa mtiifu alipokuwa mtoto. Soma Luka 2:51-52. Watu wazima walisafiri kila mwaka kwenda Yerusalemu ili kuhudhuria sherehe za Pasaka. Yesu alienda pamoja na wazazi wake alipotimiza umri wa miaka kumi na miwili. Baada ya kumaliza sherehe hiyo, kundi hilo lilianza safari ya kurudi kwao, Nazareti. Walisafiri muda wa siku nzima kabla ya kutambua kwamba Yesu hakuwa pamoja nao. Siku tatu baadaye, Mariamu na Yusufu walimpata Yesu akiwa hekaluni huku akizungumza na waalimu kuhusu Mungu. Mariamu alimwita naye akamfuata bila kulalamika. Alikuwa chini ya mamlaka ya Mariamu na Yusufu. Hii inamaanisha kwamba aliwatii.

Mungu anatwambia leo kwamba, "Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana maana hii ndiyo haki." (Waefeso 6:1)

Jaribu kutilia mkazo mambo yafuatayo unapofundisha somo hili:

1. Amri ya tano ya Mungu inatwambia tuwaheshimu wazazi wetu. Hii inamaanisha kuwapenda, kuwatii na kuwasaidia.
2. Yesu alizungumzia kuhusu watu fulani waliokataa kuwasaidia wazazi wao waliohitaji msaada.
3. Yesu aliwatii na kuwasaidia wazazi wake alipokuwa mtoto.

KUSUDI LA SOMO HILI:
Kuwaongoza wanafunzi kuweza kufikiria jinsi wawezavyo kuwaheshimu wazazi wao.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! kunaye awezaye kusimama na kukariri amri tano za kwanza? (Utapaswa kuwahimiza wanafunzi wako kujifunza kwa moyo amri tano za kwanza wiki ijayo iwapo hapatakuwa na ye yote wa kuweza kuzikariri.)

Uliza: Je! mnaona tofauti yo yote kati ya amri nne za kwanza na ya tano? (Ngojeka majibu.)

Sema: Ndiyo, amri za kwanza nne zinazungumzia kuhusu ushirika wetu na Mungu. Lakini kuanzia ya tano hadi ya kumi zinazungumzia kuhusu ushirika wetu na watu wengine. Amri ambayo tunajifunza leo inahusu uhusiano wetu kwa wazazi wetu. (Bandika amri ya tano ukutani

pamoja na zingine. Chora mstari ndefu kati ya namba nne na tano ili kuonyesha tofauti iliyoko kati yao.

Uliza: Je! Yesu alitoaje mfano wa kutii amri hii alipokuwa mtoto? (Wasimulie hadithi iliyoko katika Luka 2:41-52. Usiisome bali uisimulie. Pengine, hadithi ifuatayo itakusaidia unapojiandaa.)

Yesu alikuja duniani kama mtoto mchanga. Alikua akimsaidia Yusufu katika duka lake la useremala. Yesu alitenda yaliyo ya haki alipokuwa kijana.

Wayahudi walienda Yerusalemu kila mwaka ili kusherehekea Pasaka. Yesu alienda pamoja na wazazi wake hadi Yerusalemu alipotimia na umri wa miaka kumi na miwili.

Yesu alifurahia kuzungumza na watu waliokuwa hekaluni ambao walijua sheria za Mungu na waliowafundisha watu wengine habari za Mungu. Biblia inasema kwamba Yesu aliwasikiliza watu hawa na akawauliza maswali mengi sana. Alivutiwa sana na mazungumzo hayo hata hakujua kwamba wakati umefika wa kurudi nyumbani.

Yusufu na mamake Yesu, Mariamu, walianza safari ya kurudi nyumbani. Walidhania kwamba Yesu alikuwa kati ya marafiki na watu wa jamaa yake. Lakini hawakumpata walipoanza kumtafuta. Walirudi tena hadi Yerusalemu. Walisafiri kwa muda wa siku nzima. Mwishowe walimpata Yesu hekaluni. Alishangaa sana kwa sababu walikuwa na wasiwasi.

"Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" akawauliza. Kwa kusema Baba, alimaanisha Mungu, yaani Baba yake wa mbinguni.

Yesu alienda nyumbani kwa furaha alipoambiwa na Yusufu na Mariamu, "Ni wakati wa kurudi nyumbani." Naye aliwatii. Alitoa mfano kwa vijana na wasichana ambao wanapaswa kufuata.

(Pengine utataka kuwasaidia wanafunzi hao kuiga mchezo wa hadithi hii iwapo mna muda wa kutosha.)

(Pengine wanafunzi hawa wataona ugumu kuelewa Maandiko ya Marko 7:9-13. Mwambie wanafunzi mmoja aayasome nawe uyaeleze jinsi ifuatavyo.)

Sema: Mafarisayo waliwalaumu wanafunzi wa Yesu kwa sababu wakati mwingine hawakunawa mikono yao kabla ya chakula. Yesu aliwaambia kwamba wao walikuwa na hatia ya kosa kubwa zaidi ya hilo. Wengi wao hawakutaka kuwasaidia wazazi wao waliozeeka. Walisingizia kwamba zawadi ambazo wangepewa wazazi wao walikuwa wamezitenga kama zawadi za kumtolea Mungu. Hii ndiyo maana ya neno hili "Korbani". "Korbani" ilimaanisha kwamba sadaka au mali fulani ilikuwa imewekwa wakfu kwa ajili ya Mungu na haikupaswa kutumiwa kwa kuwasaidia wazazi waliohitaji msaada. Kwa kweli, Mafarisayo hawa walikuwa wakidanganya ili kuepuka wajibu wao wa kuwasaidia wazazi wao.

Iwapo unafundisha vijana, utapaswa kuwaelezea wajibu wao wa kuwasaidia wazazi wao kifedha. Je! ni vizuri kwa wazazi kuwatarajia watoto

wao wawasaidie mara tu wapatao kazi? Je! Yesu alimaanisha kwamba tunapaswa kuwasaidia wazazi wetu wahitajipo msaada na hawawezi kujisaidia; kwa mfano, wawapo wagonjwa na wazee kapa?

Uliza: Unawaheshimuje wazazi wako? (Jadili majibu hayo.)

Wasaidie wanafunzi na sehemu ya "Kazi ya Kufanya" iwapo wanahitaji msaada.

KAZI YA KUFANYA

Wakati mwingine ni vigumu kuwatii wazazi wako, lakini amri ya tano inasema kwamba, "Waheshimu baba yako na mama yako." Njia nzuri ya kuwaheshimu ni kuwatii.

Weka alama ya "X" kando ya kila picha iwapo utajaribu kuheshimu wakati huu.



Umemaliza chakula chako na umechoka sana. Mama yako anakwambia, "Nenda ukaoshe sufuria."



Ni siku nzuri ya kucheza na rafiki zako. Baba yako anakwambia, "Mwanangu, leo ni wakati wako wa kuchunguza mbuzi."



Unarudi nyumbani kutoka shuleni pamoja na vijana wengine. Wao wanatumia na kuzungumza maneno mabaya. Naye baba amekwambia, "Usiseme maneno mabaya hata ingawa vijana wenzako wata-kuchokoza."



WAKATI WA MWISHO

Tumia kifungu cha kukumbuka na maswali yaliyoulizwa chini yake ili kuwahimiza wanafunzi kutaka kutii wazazi wao.

Ongoza kwa maombi ambapo utawahimiza wanafunzi kutaka kuomba.

Mama amekuacha uwatunze watoto wakati aendapo sokoni. Rafiki yako anakwita mwende kucheza, lakini unakumbuka jinsi mama yako alivyokwambia, "Usimwache mtoto peke yake."

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki" (Waefeso 6:1).

Kuwaheshimu wazazi wetu inamaanisha kuwatii na kuwasaidia. Mungu ana mpango kwa jamaa na anawataka watoto wawatii wazazi wao.

Je! umtiifu kiasi gani? Je! wazazi wako wanapokwambia kitu huwa unawatii mara moja, au hungojea warudi mara nyingine? Je! uwapo peke yako na kujaribiwa kutenda jambo ovu, huwa unajiambia, "Wazazi wangu hawatagundua kamwe," au huwa unakumbuka mafundisho na kuyatii?

SURA YA TISA

KUCHUKIA NI DHAMBI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:13; Mathayo 5:21-24, 43-44; 1 Yohana 3:15-18; 4:20-21

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Hakikisha kwamba unaeleza mafundisho yako kulingana na mahitaji, shida na uelewaji wa wanafunzi wako. Iwapo mwanafunzi atauliza swali ambalo huwezi kujibu, waambie wazi kwamba hujui jibu lake, na kwamba utajaribu kutafuta jibu na utawaambia wiki ijayo.

Sheria ya Mungu ambayo tunataka tujifunze wiki hii inasema kwamba, "Usiue," (Kutoka 20:13). Biblia inazungumza juu ya kuua mtu mwingine. Haimaanishi kwamba hatupaswi kuua wanyama, ndege au samaki na kuwala kama chakula.

Hakuna aliye na haki ya kumwua mwingine. Uhai hutoka tu kwa Mungu. Mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Mwanadamu anayo roho, kwa hivyo, wakati mtu mwingine anapomwua mwenzake huwa anaiangamiza roho ambayo Mungu alimpa.

Pengine unafikiria kwamba watoto hawapaswi kujifunza juu ya amri hii. Ni watoto wachache tu ambao watafikiria juu ya kumwua mwingine. Pengine hii ni kweli. Hata hivyo, mauaji (kumwua mtu mwingine) hutokana na wivu, hasira, chuki, au tamaa ya kujichukulia nafasi ya kwanza. Hii huanzia moyoni mwa mtu.

Ni lazima uchunguze moyo wako kabla ya kutayarisha somo hili na uone iwapo una hasira na chuki yo yote. Ukiona kwamba unamchukia mtu fulani, basi utapaswa kumwomba Mungu akusamehe. Utapaswa sasa kusuluhisha mambo na mtu yule ambaye unamchukia. Soma baadhi ya vifungu kutoka kwa 1 Yohana 3 na 4. Je! una hatia ya kupenda kwa "maneno tu", bali si kwa "matendo na kweli"?

Andika amri ya sita kwenye karatasi ili uweze kuitumia wakati wa kufundisha. "Usiue" (Kutoka 20:13).

Hakikisha kwamba umetilia mkazo yale ambayo Yesu alisema katika Hotuba ya Mlimani kuhusu kuua. Soma Mathayo 5:21-24, 43-44. Yesu anasema kwamba nia zetu, mawazo na tabia ni vya muhimu sana. Mambo haya ndiyo hudhihirisha matendo yetu. Yesu anaruka kutoka kwa mipaka mikali ya barua za sheria hadi kwa roho ya sheria anaposema kwamba hatupaswi kuwakasirikia ndugu zetu, (Mtu mwingine ye yote). Alionyesha kwamba hasira na chuki ni mbegu ambazo zinaweza kuzusha mauaji iwapo hatujihadhari nazo. Yesu anasema kwamba "Tupendane". Iwapo tutapendana, basi tutakuwa tunatii amri yake isemayo, "Usiue."

Tilia mkazo mambo yafuatayo unapofundisha:

1. Amri ya sita ambayo Mungu aliwapa watu wake inatwambia

tusiue, tusichukie, na tusipange kulipiza kisasi.

2. Yesu alifundisha kwamba hatupaswi kwendelea kuwa na hasira, wala kuwachukia wengine. Alisema kwamba tunapaswa kuwapenda adui zetu, na kuwatendea mema wale wanaotuchukia.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kuelewa mafundisho ya Yesu yahusuyo matokeo ya chuki na hasira.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! amri ya sita ambayo Mungu aliwapa watu wake ni ipi? Je! amri hii inazungumzia tu juu ya kuua watu, au ni hata wanyama?

Sema: Biblia inazungumza juu ya kumwua tu mwingine. Haimaanishi kwamba hatupaswi kuwaua wanyama, ndege au samaki na kuwala.

(Bandika ukutani karatasi ambayo umeandika amri ya sita).

Uliza: Je! kwa nini hatuna haki ya kumwua mtu mwingine? (Ngojea majibu.)

Sema: Uhai hutoka kwa Mungu. Mungu tu ndiye awezaye kupana uhai. Mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Anayo roho. Wakati mtu anapomwua mwenzake huwa anaingamiza maisha ambayo Mungu alimpa.

Uliza: Je! amri hii ina maana zaidi kuliko kusema tu kwamba hatupaswi kumwua mtu mwingine? Yesu

alisemaje kuhusu amri hii? (Mchague msomaji mzuri asome Mathayo 5:21-24, 43-44.)

Siku moja, Yesu alipanda mlima pamoja na wanafunzi wake. Watu wengi walimfuata hadi kule mlimani. Walikaa chini ili wamsikilize Yesu akifundisha. Ilikuwa siku nzuri sana. Ndege walikuwa wakipaa pale angani. Nayo maua ya kupendeza yalikuwa yakipeperushwa na baridi.

Yesu akawaambia watu hao. "Waangalieni ndege wa angani. Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Yaangalie maua. Baba yenu wa mbinguni huyapa rangi nzuri za kupendeza. Baba yenu wa mbinguni atawatunza ninyi pia. Mnapaswa tu kumwamini na kuishi kwa ajili yake.

Yesu aliwaambia mambo mengi sana huku watu hao wakimsikiliza. Alitaka kuwasaidia wampendeze Mungu na wao wafurahi.

Yesu akawaambia, "Mmesikia ilivyosemwa kwamba usiue. Bali nawaambieni kwamba hampaswi kamwe kumwonea ndugu yenu hasira." Alijua kwamba baadhi ya watu huweza kuua wapatawapa na hasira.

Hatimaye Yesu akawaambia, "Basi ukileta sadaka yako mbele ya Mungu na ukumbuke ya kuwa umemkasirisha ndugu yako, basi iache sadaka yako hapo. Nenda zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako.

Pengine baadhi ya watu hao walifikiria kwamba: Mimi simchukii ndugu yangu wala sijamkosea kamwe. Ninampenda. Lakini nawachukia adui zangu.

Naye Yesu akawaambia. "Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu,

wanaombeeni wanaowaudhi" (Mathayo 5:43-44).

Uliza: Je! adui zetu ni nami? (Ngojea majibu.)

Sema: Watu wanaotuchukia na kutuudhi ndio adui zetu. Chuki huwafanya watu watake kuwaudhi wengine au hata waniue kuwaua. Biblia inasema kwamba, "Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji" (1 Yohana 3:15).



Uliza: Je! ni wangapi kati yenu ambao wanampenda Mungu? Ninyi nyote! Je! mnawapenda pia wenzenu? Hivi ndivyo Mungu anavyowataka mfanye.

Sema: Biblia inasema kwamba, "Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake ni mwongo." Inasema pia kwamba wale wanaompenda Mungu wanapaswa kuwapenda na wenzao. Wawapende hata na adui zao.

Wasaidie wanafunzi na sehemu ya "Kazi ya Kufanya." Tumia maswali haya na kifungu cha kukumbuka ili kuwelekeza ukweli wa somo hili na maisha ya wanafunzi wako.

KAZI YA KUFANYA

Andika jina lako chini ya picha inayoonyesha moyo wako.



Sentensi zilizoko upande wa kushoto hazijakamilika. Chora mstari kutoka kwa maneno yaliyoko upande wa kushoto hadi kwa yale yaliyoko upande wa kulia ambayo yatakamilisha sentensi hizi.

1. Ninajua Mungu ananipenda "Ikiwa unampenda Mungu, mpende pia ndugu yako."
2. Naweza kumpenda Mungu ambaye sija-mwona? "Nampenda Mungu," naye anamchukia ndugu yake.
3. Mtu ni mwongo iwapo atasema, kwa sababu Mwanawe alitoa maisha yake kwa ajili yangu.
4. Amri mpya ya Mungu inasema, iwapo siwezi kumpenda ndugu yangu ambaye nimemwona?"

WAKATI WA MWISHO

Jibu swali lo lote ambalo wanafunzi wanaweza kuwa nalo lihusulo somo hili.

Waongoze wanafunzi hao unapoomba au wanapoomba, ukimwambia Mungu awasaidie kwa kuwapenda wengine, hasa wale wanaowachukia na kuwaudhi.

"Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji, nanyi mnajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake" (1 Yohana 3:15).

Mwandishi wa kifungu hiki anasema kwamba chuki na mauaji ni kitu kimoja. Maneno haya yanaweza kuonekana kama ni ya kukemea, lakini Yesu hakusema tu kwamba "...mtu akiua, itampasa hukumu," bali alisema pia, "...kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu..." (Mathayo 5:21b na 22a).

Biblia inasema kwamba dhambi huleta huzuni na mauti, lakini Mungu anatupa uzima wa milele kupitia kwa Yesu Kristo. (Warumi 6:23)

Yesu ndiye Mwokozi. Hutusamehe dhambi zetu na kuziondoa tunapomwamini. Hutupa uzima ambao utaishi milele.

SURA YA KUMI

YESU ANAWASAMEHE WENYE DHAMBI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:14; Mathayo 5:27-28; Yohana 8:3-11

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Umri wao utadhihirisha jinsi utakavyofundisha somo hili. Unaweza kupata kuwa somo hili ni gumu kufundisha, hata hivyo, ni somo ambalo linastahili kufundishwa.

Kichwa kwa somo hili ni "Yesu Anawasamehe Wenye Dhambi." Utapaswa kutilia mkazo msamaha na upendo wa Mungu. Utapaswa pia kujadiliana na wanafunzi hao maana ya jamaa yenye furaha.

Ikiwa unawafundisha vijana wakubwa, pengine watakuwa na maswali kuhusu uzinzi. Wazazi wengine hawawaambii watoto wao kuhusu habari za kufanya mapenzi. Wewe kama Mkristo na mshiriki wa kanisa unapaswa kuwasaidia vijana hawa kutambua kwamba kufanya mapenzi si kubaya, ila kama kunafanya katika njia ambayo Mungu hakunua. Wasaidie wanafunzi watambue mpango wa Mungu juu ya ndoa na jamaa.

Mungu anasema katika amri ya saba kwamba, "Usizini," (Kutoka 20:14). Hii ni njia ya kusema kwamba unapooa, huwa unaahidi kumpenda na kuwa mwaminifu kwa mtu mmoja hadi wakati ambapo mtatenganishwa na kifo. Kufanya mapenzi na mtu

mwingine ambaye hajamwoa wala kuolewa ni tendo la kuzini.

Je! watu wanapaswa kutenda kulingana na ahadi ya uaminifu wao katika ndoa? Ndiyo, kwa sababu Mungu aliyapangia maisha ya jamii. Mungu alimwumba mtu wa kwanza, Adamu. Mungu akasema, "Si vyema huyu mtu awe peke yake." Halafu Mungu akamwumba mwanamke wa kwanza, Hawa. Akawaambia wazac watoto. Nao wakaanzisha jamaa ya kwanza. Nia ya mume, mke, na watoto wao kupendana na kuishi pamoja kwa furaha ilikuwa katika mpango wa Mungu. Mungu alinua kwamba mume mmoja na mke mmoja waishi pamoja katika ndoa na waaminiane.

Je! Yesu alifundisha nini kuhusu amri hii isemayo, "Usizini?" (Soma Mathayo 5:27-28)

Yesu alisema kwamba tunaweza kuwa na hatia ya kuzini kulingana na vile tunavyojisikia mioyoni mwetu kuhusu mtu mwingine. Uzinzi huanza kwa tamaa mbaya iliyoko katika akilini na mioyoni mwetu.

Yesu hakuvumilia dhambi, hali alionyesha upendo kwa wenye dhambi. Soma Yohana 8:3-11. Yesu hakukubaliana na yale ambayo mwanamke huyu alikuwa amefanya. Lakini alikuwa tayari kumsamehe.

Andika amri ya saba isemayo, "Usizini," na uibandike ukutani

unapofundisha somo hili. Unapaswa uwe na amri saba ukutani au kwenye ubao sasa. Waongoze wanafunzi katika kuvikariri.

Kumbuka ukweli muhimu ufuatao unapojiandaa kufundisha.

1. Amri ya saba ya Mungu inasema kwamba mume na mke wanapaswa kuaminiana.
2. Yesu alisema kwamba ni dhambi kwa mtu kufikiria kufanya maovu, kwa sababu ni sawa tu na kutenda jambo lenyewe.
3. Yesu alimsamehe mwanamke aliyekuwa amefanya maovu, naye ataweza kutusamehe pia.
4. Matakwa ya Biblia ni kwamba kufanywa mapenzi kumetengewa mume na mke waliooana.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kuelewa mpango wa Mungu kwa jamaa na watambue mafundisho ya Yesu yasemayo kwamba matendo ya dhambi hutokana na mawazo mabaya.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! umewahi kuhudhuria arusi? Wakati mwingine arusi hufanyika kijijini ambako bibi arusi huishi. Wakati mwingine hufanyika kanisani. Arusi huwa ni wakati wa furaha. Sherehe ya arusi ni njia ya kuwaambia majirani na watu wengine kwamba watu wawili wanaanza maisha ya pamoja.

Uliza: Je! mpango wa Mungu ni upi kwa jamaa? (Ngoja majibu.)

Sema: Mungu alipangia kuwepo kwa maisha ya jamii. Mungu ndiye aliyemwumba mtu wa kwanza, Adamu. Mungu akasema, "Si vyema huyo mtu awe peke yake." Halafu akamwumba pia mwanamke wa kwanza, Hawa. Akawaambia wazac watoto. Nao wakaanzisha jamaa ya kwanza. Nia ya mume na mke na watoto wa kupendana na kuishi pamoja kwa furaha ilikuwa katika mpango wa Mungu.

Uliza: Je! kwa nini hakuna furaha katika baadhi ya jamaa, iwapo ilikuwa nia ya Mungu kwa wao kuishi pamoja kwa furaha? (Jadili)

Sema: Jamaa nyingi hazina furaha kwa sababu watu wenyewe hawaishi kulingana na mpango wa Mungu wa kuwa na furaha. Huvunja ndoa yao kuwa na furaha. Huvunja ndoa yao kwa kusahau ahadi yao ya ndoa. kufanya mapenzi na mke mwingine badala ya yule aliyemwoa. Naye mke anaweza kutoroka na mume mwingine. Au mume anaweza kuoa wake zaidi ya mmoja. Mpango wa Mungu ni kwa mume mmoja kumwoa mke mmoja hadi watakapo-tenganishwa na kifo.

Sema: Kwa kweli, nyinyi jinsi mliyvyo mngali wadogo sana wa kuweza kuoa au kuolewa. Lakini nyingi si vijana sana wa kutoweza kujiamulia iwapo mnataka kufuata mpango wa Mungu baadaye ili mwe na ndoa yenye furaha iwapo amewapangia kuoa au kuolewa.

Sema: Sasa hebu tuone yale ambayo Yesu alisema kuhusu amri ya saba.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Mathayo 5:27-28.

Uliza: Yesu alisemaje kuhusu umuhimu wa mawazo na tamaa za mtu?

Sema: Yesu alisema kwamba tunaweza kuwa na hatia ya kuzini kulingana na vile tunavyojisikia mioyoni mwetu kuhusu mtu mwingine. Uzinzi huanzia kwa tamaa ambayo iliyoko akilini na mioyoni mwetu. Kila mmoja wetu anapaswa kujihadhari na jinsi afikiriavyo. Mawazo mabaya yanaweza kuja akilini mwetu, lakini tunaweza kuyabadilisha kwa kufikiria mambo mema.

Uliza: Je! kuna tofauti gani kati ya mawazo na matendo? Je! mnaona jinsi ilivyo muhimu kuwa na mawazo mema?

Sema: Hebu sasa tusikilize hadithi ya Yesu jinsi alivyomsamehe mwanamke aliyekuwa amezini. (Simulia hadithi iliyoko katika Yohana 8:3-11 kwa kutumia maneno yako mwenyewe. Muhtasari ufuatao utakusaidia.)

Siku moja watu fulani walimpeleka mwanamke mmoja kwa Yesu. Mwanamke huyu alikuwa amependa mume ambaye hakuwa wake, na watu hawa walimtaka Yesu amlaumu kwa jambo hilo. Wakamwambia, "Bwana, mwanamke huyu amepatwa akikosa. Hapo kale Musa alisema kwamba tupige kwa mawe mwanamke kama huyu. Nawe unasemaje?"

Yesu alimsikitikia sana mwanamke huyu. Akawaangalia watu wale na akawaambia, "Yeye asiye na dhambi

miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe." Halafu akainamisha kichwa chake na akaanza kuandika mchangani.

Yesu alijua kwamba watu hawa wote walikuwa wamekosa maishani. Hakuna aliyethubutu kumtupia jiwe mwanamke yule. Walianza kuondoka kimyakimya.

Yesu akainua kichwa chake. Akamwuliza mwanamke yule; "Wako wapi washtaki wako? Je! hakuna aliye kuhukumu kuwa na hatia?" Mwanamke yule akamjibu, "Hakuna Bwana."

Halafu Yesu akamwambia, "Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako wala usitende dhambi tena."

Uliza: Yesu alimtendeaje mwanamke aliyoko katika hadithi hii?

Sema: Alikuwa mpole kwake. Alikuwa ametenda dhambi. Alikuwa amefanya kosa. Lakini alisikitikia na kukiri dhambi zake, naye Yesu akamsamehe. Yesu hakusema kwamba ilikuwa vyema kwake kufanya dhambi. Alijua kwamba alikuwa amekosa lakini alimsamehe na kumwambia asifanye dhambi tena.

Sema: Ni furaha ilioje kwamba Yesu alimsamehe mwanamke huyu mwenye dhambi? Tunajua kwamba atatusamehe hata nasi. Biblia inasema kwamba watu wote wamefanya dhambi, au wamekosa. Hii inamaanisha kwamba sisi pia, tumefanya dhambi. Yesu atatusamehe iwapo tutasikitika na kukiri makosa yetu. Biblia inasema kwamba, "Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu." (1 Yohana 1-9)

Uliza: Ni lazima tufanyeje iwapo tunamtaka Yesu atusamehe dhambi zetu?

Sema: Ni lazima tutubu iwapo tunamtaka Yesu atusamehe dhambi zetu. Hii inamaanisha kwamba ni lazima tumwambie kuwa tumefanya dhambi. Si rahisi kumwambia Yesu kwamba tumekosa kumtii au tumevunja mojawapo ya amri zake. Lakini atatusamehe iwapo tutamwambia kuwa tumekosa na tumwombe msamaha.

Wape wanafunzi muda wa kuuliza maswali yote waliyonayo. Pengine utataka wakati huu kuzungumza juu ya matatizo ambayo wanafunzi hao wanayo yahasuyo ukweli wa somo hili.

Wasaidie wanafunzi na sehemu ya "Kazi ya Kufanya." Rudieni kifungu cha kukumbuka pamoja na vifungu vingine.

KAZI YA KUFANYA

Je! umewahi kuandika ujumbe kwa kutumia mpango wa herufi? Utapata hapo chini maneno ya kifungu cha kukumbuka cha leo ambayo yameandikwa kwa namba. Jaribu kuyatambua ni yapi, halafu uandike neno linalofaa katika nafasi iliyoachwa.

Mpango huu wa herufi ni:

A = 1	J = 10	S = 19
B = 2	K = 11	T = 20
C = 3	L = 12	U = 21
D = 4	M = 13	V = 22
E = 5	N = 14	W = 23
F = 6	O = 15	X = 24
G = 7	P = 16	Y = 25
H = 8	Q = 17	Z = 26
I = 9	R = 18	

Mungu anasema katika Biblia kwamba, "Hatimaye, ndugu zangu, mambo yale yaliyo ya 11-23-5-12-9 KWELI, yo yote yaliyo ya 19-20-1-8-1 STAHA, yo yote yaliyo ya 8-1-11-9 HAKI, yo yote yaliyo ya 19-1-6-9 SAFI, yo yote yenye 11-21-16-5-14-4-5-26-1 KUPENDEZA, yo yote yenye 19-9-6-1 SIFA njema, ukiwapo 23-5-13-1 WEMA wote, ikiwapo 19-9-6-1 14-26-21-18-9 SIFA NZURI yo yote yatafakarini hayo" (Wafilipi 4:8).

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi; yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema, ukiwapo wema wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote yatafakarini hayo" (Wafilipi 4:8).

Yesu alipozungumzia kuhusu amri ya saba alisema kwamba ni dhambi hata kufikiria mawazo mabaya akilini mwako. Alisema hivi kwa sababu

wakati mtu ANAPOFIKIRIA
mawazo mabaya kwa muda mrefu,
huanza KUTENDA kulingana na
fikira zake.

Je! unawezaje kujizuia kutofikiria
mawazo mabaya? Neno la Mungu
linatupa siri moja katika kifungu cha
kukumbuka cha leo. Je! siri hiyo ni
ipi?

WAKATI WA MWISHO

Pengine wanafunzi wataona haya ya
kuuliza maswali kwa hivyo utapaswa
kuwatia moyo ili waulize. Wewe kama
mwalimu wao unapaswa kujua
mahitaji na shida zao. Wasaidie
kupata majibu ya Mungu.

Funga kwa maombi.

SURA YA KUMI NA MOJA

KUIBA NI DHAMBI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:15; Luka 19:1-10; Marko 12:38-40; Amosi 8:4-5

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Amri hii ya nane, "Usiibe" inaweza kuwa mojawapo ambayo wanafunzi wako wataona ni ngumu kuitii. Wanaweza kuchanganyikiwa kuwa ni wakati gani ambapo mtu hufikiriwa kuwa anaiba. Unapaswa kuwasaidia waelewe kwamba hawatakiwi kamwe kuchukua kitu cho chote ambacho ni cha mwingine. Haijalishi iwapo kitu hicho ni kidogo au hakina dhamani kubwa, au iwapo ni cha thamani kubwa. Ni vibaya kuchukua kitu ambacho ni cha mtu mwingine.

Wasaidie watoto waelewe kwamba wizi ni wa aina nyingi. Wakati mtu anapodanganya katika biashara yake huwa anaiba. Wakati Mkristo anapokosa kutoa zaka na sadaka huwa anamwibia Mungu. Kupokea hongo ni wizi. Kudanganya shuleni ni wizi.

Hebu chunguza maisha yako mwenyewe na uone kama umwaminifu katika mipango yako na wengine.

Wasaidie watoto waone wajibu wao wa kupunguza wizi unaoendelea katika taifa lao, hasa mijini.

Soma Luka 19:1-10. Hadithi ya Zakayo ni mfano mzuri jinsi mtu awezavyo kuiba bila kuvunja na kuingia katika nyumba ya mwenzake jinsi waizi wafanyavyo.

Zakayo alikuwa tajiri sana. Alitajirika kwa kutosha ushuru mwingi kuliko ilivyompasa. Alichukua zile pesa alizopata zaidi. Hali hakuwa na furaha.

Aliweza tu kuwa na amani moyoni mwake baada ya kukutana na Yesu na kuamua kumpendeza yeye. Aliwapa wale watu aliowaibia mara nne zaidi ya mali yao aliyochukua. Alibaki sasa na pesa chache lakini akawa na amani na Mungu, ambayo ilikuwa bora zaidi.

Soma Marko 12:38-40 ili uone yale ambayo Yesu alisema kuhusu udanganyifu wa baadhi ya waandishi.

Waandishi hawakuiba pesa. Bali walikuwa wadanganyifu katika kazi zao. Waliendelea kuwa matajiri hali wajane waliojidai wanawasaidia wakiwa maskini. Waandishi hawa walitaka tu wenzao waseme kuwa walikuwa watu wema. Walitaka kuambiwa wao walikuwa wakimcha Mungu, wafuasi wa dini na wema. Hali Yesu alisema, "Jihadharini na waandishi!" Walitenda kinyume cha yale waliyosema.

Sasa soma Amosi 8:4-5.

Kuna njia nyingi za kutotii amri hii isemayo, "Usiibe". Mfanya biashara anaweza kuwaibia wanunuzi wake wakati ambapo hawaambii bei kamili. Pengine atataka pesa za kilo mbili ya nyama, hali anawapimia tu kilo moja na nusu. Mwanamke anayeenza mboga anaweza kuweka zile zilizooza chini ya

ngunia ili zisionekane. Hivyo ni kutokuwa mwaminifu na ni kuiba. Hapo kale wakati Amosi alipokuwa nabii, wafanya biashara hawakuwa waaminifu. Waliweka kipimo siyo ya kweli ili watoe vifaa vidogo kuliko zile watu walizonunulia: Hii ilikuwa njia moja ya kuiba naye Mungu hakuwafurahia kamwe.

Tilia mkazo mambo haya unapofundisha:

1. Amri ya nane inasema, "Usiibe." Kulingana na Mungu hakuna sababu ifaayo ya kutotii Neno lake.
2. Zakayo alirudisha mali yote aliyokuwa amewaibia maskini, alipokuwa mfuasi wa Yesu Kristo.
3. Amosi, nabii wa Mungu, alizungumza juu ya watu wa Mungu kwa sababu walikuwa wakidanganya na kuiba.

Andika amri hii kwenye karatasi jinsi ulivyoandika zile zingine. Waonyeshe unapozanza kufundisha.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwaongoza wanafunzi kuweza kugundua maana ya "kuiba" iliyoko katika Biblia.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! wizi ni nini? (Wape muda wa kujibu.) Tazama ufafanuzi wa neno hili ulioko katika somo la wanafunzi. Jadili juu ya tofauti iliyoko kwa matumizi kati ya kitu cha jamaa yote au ukoo na kitu cha mtu binafsi.

Uliza: Je! kwa nini watu kuiba? Unapaje juu ya sababu zifuatazo ambazo watu hutoa baada ya kuiba?

1. Kwa sababu ya njaa
2. Kwa sababu ya kujaribiwa na marafiki wabaya
3. Kwa sababu ya tamaa
4. Kwa sababu ya uvivu
5. Kwa sababu ya kuwa maskini hali wengine wana mali nyingi. (Jadiliana mambo haya yote.)

Uliza: Biblia inasemaje kuhusu kuiba? (Waambie wanafunzi kadhaa watafute vifungu hivi na wavisome. Kutoka 20:15. Warumi 12:17, Malaki 3:8, Amosi 8:5; Marko 12:40.)

Sema: Yesu humbadilisha mtu wakati anapompokea kama Mwokozi wake. Mtu huyo atataka kutenda mema, kuwa mwaminifu na kumpendeza Yesu.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Luka 19:1-10. Au, unaweza kuelezea habari hii kwa maneno yako mwenyewe wakati wanafunzi wanaposoma Biblia zao. Ukitaka, unaweza kuwaambia wanafunzi waigie mchezo wa hadithi hii ya Zakayo.

Uliza: Je! ni nini kilichofanyika kwa Zakayo alipoamua kumfuata Yesu? (Tazama kifungu cha 8)

Sema: Yesu hutufanya tuishi maisha ya haki aingiapo moyoni mwetu. Hutufanya tutake kuwa waaminifu. Huwa hatutaki kuiba wakati Yesu

aingiapo moyoni mwetu. (Mchague mwanafunzi wa kusoma Amosi 8:4-5)

Sema: Amosi, nabii wa Mungu, aliwaambia watu wa Mungu kwamba walikuwa wakikosa katika matendo yao. Alisema kwamba, walikuwa wakiwaibia maskini na hawakuwa waaminifu waliponunua na kuuza. Mungu alichukizwa sana kwa sababu watu wake walikuwa wakifanya mambo haya!

Mwambie mmoja wao asome Marko 12:38-40.

Uliza: Yesu alisemaje kuhusu viongozi wa kidini ambao waliji-onyesha wakati wa kuabudu hali walikuwa wadanganyifu? (Jadili)

Soma: Ndiyo, Yesu aliwafahamu vyema watu hawa. Alisema kwamba walifurahia walipoonwa na watu na kuzungumza nao kila mara. Walikaa kila mara mahali pazuri. Lakini waliwaibia wajane, na kuomba sala ndefu na kujifanya kuwa ni wema. Lakini wataadhibiwa.

Sema: Wakati mwingine watu waibapo, wengine huwa hawajui. Lakini Mungu hujua na hataki wajifanye kuwa ni wema.

Uliza: Je! unafikiri kwamba watu wachukua hongo huwa wanaiba? (Jadili tatizo la kupokea hongo. Ni njia ya kuiba kwa sababu wakati mtu maisha yake. Jamii hii, kanisa, udiyo ambacho si halali.)

Wasaidie wanafunzi na sehemu yao ya "Kazi ya Kufanya."



KAZI YA KUFANYA

Kuna watu wawili katika picha hii. Andika jina la kila mmoja chini ya picha hiyo. (Wanafunzi hao wanapaswa kuandika ZAKAYO chini ya mtu aliyeko juu ya mti na YESU chini ya mtu aliyesimama.)

Je! yule mtu aliyesimama chini anamwambiaje yule aliyekaa mtini? Andika maneno yenyewe katika nafasi ifuatayo. Utayapata katika Luka 19:5.

"Zakayo, shuka upesi, kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako."

Je! mtu yule aliyepanda mtini alifanyaje? (Luka 19:6)

Alishuka chini kwa haraka na kumkaribisha Yesu nyumbani kwake.

Je! alikuwa na hatia ya dhambi ipi?

Dhambi ya kuiba.

Alifanyaje alipotubu dhambi zake na kusamehewa? (Luka 19:8)

Alirudisha mara nne zaidi ya mali za watu alizokuwa amechukua na akawapatia maskini nuru ya mali yake.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Mwibaji asilibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kungawia mhitaji” (Waefeso 4:28).

Ikiwa kweli tunamfuata Yesu hatuwezi kuendelea kutokuwa waaminifu. Ikiwa tumeiba ni lazima turudishe au tulipie kile tulichoiba. Ni lazima tufanye yaliyo mema mbele ya Mungu na mwanadamu.

WAKATI WA MWISHO

Waongoze wanafunzi katika kumwomba Mungu msamaha iwapo hawajakuwa waaminifu kwa hali yo yote. Waongoze katika kuombea jambo hilo.

SURA YA KUMI NA MBILI

SEMA UKWELI KILA MARA

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:16; Mathayo 12:33-37; Waefeso 4:15, 29-31

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Watoto hudanganya mara nyingi ili waepuke adhabu. Wengine hudanganya ili wasikilizwe au wahurumiwe. Wengine hudanganya ili waonekane wema hali wenzao wachukuliwe makosa. Wasaidie wanafunzi hao kuona kwamba inaweza kuwa vigumu kuacha baada ya kuzoea kudanganya. Wasaidie kuelewa kwamba hakuna awezaye kuwaamini iwapo watazoea kudanganya.

Je! unaufahamu mzuri juu ya amri hii isemayo, "Usimshuhudie jirani yako uongo" (Kutoka 20:16)? Tunaweza kusema kwamba amri hii inamaanisha kwamba: Utapaswa kusema ukweli wakati wote na mahali po pote ulipo. Neno hili "jirani" jinsi lilivyotumiwa hapa halimaanishi tu kwamba yule aishiye karibu nawe, bali ni mtu ye yote.

Sisitizo ya somo hili linapaswa kuwa kwamba yale mtu asemayo hutegemea hali ya moyo wake. Yale mtu afikiriayo, asemayo na afanyayo yatakuwa mema iwapo amepatania "kindani" na Mungu.

Soma Mathayo 12:33-37. Yesu alikuwa akiangalia ndani ya moyo wa mtu alipokuwa akizungumzia kuhusu dhambi. Je, umetambua kwamba wakati Yesu alipofafanua amri hizi

alianzia kwanza na mawazo na hali ya mtu? Mtu hudanganya kutokana na moyo usiomsafi.

Paulo alipinga vikali Wakristo ambao hutumia vibaya midomo yao. Soma Waefeso 4:15, 29-31.

Soma somo lote lililoko katika kitabu cha wanafunzi.

Tayarisha vifaa vya kufundishia. Andika kifungu cha Kutoka 20:16 kwenye karatasi ili ukitumie unapofundisha.

Tilia mkazo mambo haya unapofundisha:

1. Amri ya tisa ya Mungu inasema kwamba hatupaswi kumshuhudia jirani yetu uongo. Hii inamaanisha kwamba hatupaswi kudanganya kamwe.
2. Yesu alisema kwamba maneno mema hutoka katika moyo msafi hali maovu hutoka katika moyo mbaya.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia watoto waelewe sababu zinazowafanya watu wadanganye na kuwahimiza watake kusema ukweli.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! umewahi kusema maneno ya ukali kuhusu wengine? Bila shaka kila mmoja wetu afanya hivyo. (Wasimulie hadithi ifuatayo.)

Siku moja mtu mmoja alisema maneno yasiyo ya upole na yasiyo ya kweli kuhusu

jirani yake. Mwishowe alijisikitikia sana na akamwuliza mtu mmoja jambo la kufanya.

Mtu yule alimwambia aangushe unyoya laini katika kila mlango wa nyumba iliyoko katika kijiji hicho. Alifanya jinsi alivyoambiwa. Hatimaye yule mwenye ujasiri alimwambia arudi na akakusanye tena mahyoya hayo yote. Mtu huyo akamwambia, "Siwezi nikayakusanya. Baridi imepeperusha mahyoya yote."

Yule jasiri alivyosikia haya, akamwambia, "Maneno mema na mabaya husemwa kwa urahisi, lakini hayawezi yakarudi tena."

Sema: Mdomo ni sehemu muhimu ya mwanadamu. Mdomo husema yale ambayo tunafikiria moyoni mwetu. Mdomo wa mtu yule ambaye moyo wake umejaa maovu husema maneno mabaya kama ya kulaani, uongo na kuzusha uvumi - masengenyo. Lakini moyo wa yule ampendaye Mungu na kutaka kumpendeza husema ukweli kwa njia ya upendo.

Sema: Yesu alikuwa akiangalia ndani ya moyo wa mtu alipokuwa akizungumzia kuhusu dhambi. Hebu tusome Mathayo 12:33-37 na tuone yale ambayo Yesu alisema hutoka kinywani mwa mtu.

Uliza: Je! ni tunda lipi unalopata kwenye mti wa mwembe? Ndiyo, utapata maembe.

Uliza: Je! ni nini kipatikanacho kwenye mti wa miba? Miba ndiyo hukua kwenye mti huo.

Uliza: Je! ni nini kitokacho ndani ya moyo wako? Je! kifungu cha 35 kinasemaje? ("Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema; na mtu

mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya" (Mathayo 12:35)).

Sema: Hakuna ye yote kati yetu aliye na moyo mzuri. Kila mmoja amefanya dhambi. Yesu Kristo amemwaga damu yake ili tuweze kusafishwa na kutakaswa. Ni wakati tujapo tu kwake kwa imani na kumwomba atutakase ndipo tuwapo na moyo safi.

Uliza: Je! mnafikiri kwamba wakati mwingine Wakristo huacha maneno mabaya yatoke kinywani mwao?

Sema: Hebu tufungue katika Waefeso 4 na tutafute jibu lake. (Mwambie mmoja asome kifungu cha 15 na mwingine asome kuanzia 29-31. Jadili vifungu hivi.)

Uliza: Je! amri ya tisa inasemaje? (Waonyeshe karatasi ambayo umcandika amri ya tisa. Waambie warudie kifungu hicho pamoja.)

Uliza: Je! mnafikiri amri hii inamaanisha nini? (Jadili majibu yao.)

Uliza: Je! Mungu hukubaliana na uongo hata ukiwa ni "mdogo" sana? (Jadili)

Uliza: Je! huwa tunatumia njia zipi kwa kudanganya? (Jadili) Je! huwa tunaharibu nini tunapodanganya? (Tunaharibu uaminifu wetu. Hakuna ambaye atategemea yale tusemayo).

Neno la Mungu linatwambia jinsi Mungu anavyochukia uongo. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome Mithali 12:22)

Jadiliana kifungu cha kukumbuka. Wasaidie wanafunzi na sehemu ya "Kazi ya Kufanya.")

KAZI YA KUFANYA

Umeelewaje maana ya Maandiko yaliyoko katika somo hili?

Kuna sentensi katika upande wa kulia wa sehemu hii zinazozungumzia kuhusu Maandiko ya leo na ambazo hazina neno moja. Chagua neno lifaalo kutoka kwenye orodha iliyoko upande wa kushoto.

- | | |
|--------|---|
| moyo | 1. Amri ya tisa inasema kuwa, " <u>U</u> simshuhudie <u>jirani</u> yako uongo." |
| ukweli | 2. Yesu akawaambia, "Maana kinywa cha mtu huyanena yaujazayo <u>moyo</u> wake." |
| jirani | 3. Paulo aliwaambia Wakristo wa Efeso kusema <u>ukweli</u> kwa moyo wa upendo. |

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Basi uvuoni uongo, mkasamehe kweli kila mtu na jirani yake..." (Waefeso 4:25).

Kusema uongo juu ya wengine huzusha shida. Huleta uchungu moyoni. Maneno ya uongo yanaweza kuharibu sifa ya mtu mwingine.

Ikiwa sisi ni watu ambao hatuwaambii ukweli jirani zetu, basi wao hawawezi wakatuamini.

Kusema uongo hutoka kwa moyo uliojaa uongo. Dhambi yo yote

huanza katika moyo ambao haushirikiani na Mungu. Ikiwa mioyo yetu imejaa wema na upendo wa Mungu, itajazwa pia na upendo na wema kwa watu wengine.

WAKATI WA MWISHO

Waongoze wanafunzi katika kumwomba Mungu awape mioyo misafi na miema. Hapo kale Daudi aliomba kwamba, "Ee Mungu, uniumbie moyo safi." (Zaburi 51:10)

Tumia kifungu hiki kama ombi la mwisho.

SURA YA KUMI NA TATU

HATUPASWI KUWA WACHOYO

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:17, Luka 12:13-31

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! wanafunzi wako wamefurahia mafunzo haya ya Amri Kumi? Je! wameelewa jinsi Yesu alivyofafanua sheria hii? Je! wamepata uelewaji mwema wa ujumbe wa Biblia? Bila shaka jibu la maswali haya yote ni "Ndiyo."

Utapaswa kuwatia moyo wanafunzi hao wakariri Amri Kumi hizi unapokaribia mwisho wa somo hili. Pengine utapanga kuwa na mashindano ya kumwona yule awezaye kukariri amri zote kumi.

Wanafunzi wengi hawatajua maana ya neno "kutamani" ambalo limetumiwa katika amri hii ya kumi. Uwe tayari kuwaelezea maana yake.

Rudia masomo matatu ya kwanza ya mfululizo wa masomo haya utakapojitayarisha kufundisha. Je! unaona jinsi Amri Kumi zilivyo sehemu ya agano ambalo Mungu alifanya na watu wake?

Utapaswa kusoma Maandiko mengine mbali na yale uliyopewa. Je! uaelewa maana halisi ya kutamani? Je! unajua yale Biblia isemayo kuhusu dhambi hii? Soma Maandiko yafuatayo. Ezekiel 33:31; Mika 2:2; Habakuki 2:9; Wakolosai 3:5; 2 Samweli 12:1-10.

Mfano ambao Yesu alitumia katika Luka 12 ni mzuri sana. Unaonyesha

kile kifanyikacho wakati mtu huwa mchoyo na kutaka tu aongezwe zaidi na zaidi. Soma kuanzia kifungu cha 13 hadi 31.

Andika amri hii kwenye karatasi na uongezee kwa zile ambazo umebandika ukutani, darasani humo.

Tilia mkazo ukweli huu ufuatao unapofundisha.

1. Amri ya Kumi ya Mungu inawaambia watu wake wasitamani au kutaka kile ambacho jirani yao anacho.
2. Yesu alisimulia hadithi ihusuyo mkulima aliyetajiri ambaye alikuwa na mali nyingi kuliko vile alivyohitaji. Lakini alikuwa mjinga. Alitaka apate mali nyingi zaidi kuliko ile aliyokuwa nayo.
3. Tamaa inatokana na uchoyo.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kutambua matokeo ya kutamani.

KULIFUNDISHA SOMO

Bandika ukutani karatasi uliyoandika amri hii, "Usitamani nyumba ya jirani yako."

Sema: Iangalieni amri hii ya mwisho. Inasema kwamba, "Usitamani."

Uliza: Je! inamaanisha nini kutamani? (Jadiliana majibu haya.)

Sema: Kutamani inamaanisha kutaka kitu ambacho ni cha mtu mwingine. Inamaanisha pia kwamba kutaka kitu kingine mbali na kile ulichonacho. Ni kuwa mchoyo na vitu ulivyonavyo.

Uliza: Je! ni wangapi kati yenu walio na vitu ambavyo wanavithamini sana? Kinaweza kuwa kitabu kizuri, au baiskeli au mpira. Je! huwa unawapatia wenzako? Iwapo tuna moyo ambao tunataka kile kilicho na wenzetu, basi hata nasi tu wachoyo pia. Pengine hatutaki kuwapatia wenzetu kile tulichonacho. Amri hii inazungumza juu ya aina ya yote ya uchoyo. (Jadili juu ya uchoyo na kutotaka kuwapatia wenzetu vitu ulivyonavyo.)

Sema: Wakati watu wanapotamani au kutaka kile ambacho wenzao wanacho, huwa hawana furaha. Hawatosheki na vile walivyonavyo. Siku moja Yesu alisimulia hadithi ya mkulima mmoja tajiri aliyekuwa na mali nyingi kuliko alivyohitaji.

Unaweza kuwachagua baadhi ya wanafunzi wasome Luka 12:13-31, au unaweza ukasimulia hadithi hii. Wasaidie wanafunzi kuiga mchezo wa hadithi hii iwapo mna muda wa kutosha. Pengine habari ifuatayo itakusaidia iwapo utaamua kusimulia hadithi hii kwa wanafunzi.

Shamba la mkulima mmoja lilikuwa na mazao mengi ya mahindi na ngano. Alikuwa na chakula kingi sana hata hakujua mahali pa kukihifadha.

"Nitafanyaje," akawaza. "Ghala zangu zimejaa. Sina mahali pa kuweka chakula changu chote."

Mkulima huyu hakumfikiria Mungu kamwe, au kumshukuru kwa ajili ya chakula hicho. Hata hakufikiria kuwapatia maskini baadhi ya chakula hicho. Akasema, "Nitavunja ghala zangu na nijenge zingine kubwa. Halafu nitaweka chakula changu chote humo. Sitafanya tena kazi kwa bidii. Nitakuwa tu na maisha mazuri na yenye furaha."

Lakini mkulima huyu tajiri hakuwa na maisha yenye furaha. Mungu akamwambia, "Wewe ni mpumbavu sana. Utakufa usiku wa leo. Je, vitu hivi ulivyojiwekea vitakuwa vya nani?"

Baada ya Yesu kusimulia hadithi hii, alisema kwamba, "Ndiyo ilivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba asijitayarisha kwa Mungu."

Sema: Watu huwa wakarimu kwa Mungu iwapo wanampenda na kumtumikia Mungu na kuwasaidia wengine. Wao hujiwekea akiba ya hazina zao kule mbinguni. (Jadiliana maana ya "utafuteni kwanza ufalme wa mbinguni.")

(Wasaidie wanafunzi na sehemu ya "Kazi ya Kufanya" na uwaelezee maana ya kifungu cha kukumbuka.)

KAZI YA KUFANYA

Aya ifuatayo ina habari za yule mkulima tajiri. Baadhi ya sentensi zake si za kweli. Piga mstari chini ya sentensi zote ambazo ni za kweli. Sasa soma sentensi zote ulizopiga mstari na uone kama zinasimulia hadithi iliyoko katika Luka 12:16-21.

Mkulima mmoja tajiri alikuwa na shida. Ghala zake zilikuwa ndogo sana. "Nitafanyaje," akawaza. "Sina nafasi ya kutosha mavuno yangu."

Halafu akawakumbuka wajane na mayatima watiomaskini. Akaamua kuwapatia chakula. Akajiwa na wazo: "Nitavunja ghata zangu na nijenge zingine kubwa zaidi." Aliamua kuuza mavuno yale na alipatia kanisa pesa atakazopata. Alifikiri kwamba hana jambo lingine la kuwazia. Alikuwa na pesa nyingi. Kuanzia wakati huo, alifikiria kwamba atakula, anywe na kufurahia tu. Mungu akamwambia, "Nimefurahi kwa sababu unafikiria pale ambapo utaishi milele." Mungu alimwita mtu huyu mpumbavu kwa sababu hakuwa na Mungu maishani mwake. Mtu huyu alikufa usiku huo huo. Mfikirie Mungu kwanza naye atakutunza.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Angaliwa, Mlindeni na choyo"
(Luka 12:15a).

Mungu hatutaki tuwe wenye tamaa au wachoyo. Anatutaka tushiriki na wenzetu vitu vyema tulivyonavyo.

Je! unajua jinsi watu wengine hushika nyani? Hutoboa tundu kwenye buyu. Tundu hiyo huwa tu kiasi cha kumwezesha tu nyani yule apitishie mkono wake. Halafu hujaza njugu katika buyu hilo nakulifungia juu ya mti.

Nyani yule huingiza mkono wake katika tundu hilo na kuchukua njugu mkononi mwake. Sasa huwa hawezi kutoa mkono wake nje kwa sababu hataki kuachilia njugu zile. Yeye hukaa tu hapo hadi wale watu waliomtega warudipo na kumkamata.

Watu wenye tamaa wako kama nyani huyu. Hawawezi kuachilia kitu cho chote walichonacho. Wanataka kujiwekea akiba yote.

Hebu tuombe na tumwambie Mungu atusaidie tusiwe watu wenye tamaa, lakini tufurahie kushiriki na wenzetu vitu tulivyonavyo.

WAKATI WA MWISHO

Rudia amri zote. Wahimize wanafunzi wako wakariri amri hizo zote.

Omba kwamba mafunzo haya yatawasaidia wanafunzi hao kujua yale ambayo Mungu anawatarajia wafanye. Omba kwamba watatumia nguvu ambazo Mungu atawapatia kwa kuwasaidia watii amri zote.